Nipashe
Jumatatu Januari 15, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581556
0745 700710 LIKE & FOLLOW US
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital | epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com



WACHEZAJI 7 BORA 2023

UKURASA 12



Mkurugenzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Mrisho Mrisho

# Meli zafurika bandarini Dar

• **Watendaji** 'meno nje', 16 zingine kutia nanga leo...

*Endelea ukurasa 2*



Bandari ya Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

## Mvua yafukua makaburi, miili yazikwa tena

UKURASA 16



MSIMAMO WA CHADEMA

## CCM yaibuka na lake kwa Mbowe na Tundu Lissu

UKURASA 3

UKURASA WA 2

**UN** yatoa angalizo kwa serikali sheria za uchaguzi

UKURASA WA 9

MAPOROMOKO HANANG

**Wajasiriamali** wenye bima walipwa fidia mamilioni ya shilingi

UKURASA WA 18

**RITA** yamaliza zogo usajili wa ndoa za serikali

**MICHEZO** **BENCHIKHA ATAKA STRAIKA WA MABAO** UK.24 **KATUNI** UK.6

# Umoja wa Mataifa watoa angalizo sheria za uchaguzi

Na Jenifer Gilla

WAKATI Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ikipokea maoni kutoka kwa wadau kuhusu marekebisho ya miswada minne ya sheria zinazohusu uchaguzi, Umoja wa Mataifa (UN) umetoa angalizo kuhusu mchakato huo.

Miswada hiyo ni ya: Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023; Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023; Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 5 wa Mwaka 2023; na Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023.

Tanzania ikiendelea na mchakato huo wa marekebisho ya sheria, UN imeitaka kuzingatia makubaliano yaliyopo katika mikataba ya kimataifa na kikanda iliyoyaridhia kwa kuyatia saini.

UN imekumbusha kuwa mikataba hiyo inaelekeza nchi wanachama, ikiwamo Tanzania, kuchukua jitihada za makusudi za kisheria na kisera kufikia uwiano wa 50:50 kwa wanawake na wanaume katika nafasi za uongozi na vyombo vya kufanya uamuzi.

Kupitia shirika lake la wanawake (UN Women) chini ya Mkurugenzi Mkazi Hodan Addou, UN ilitoa angalizo hilo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam ilipowasilisha kwa waandishi wa habari matokeo ya uchambuzi wake kuhusu miswada hiyo.

UN Women kwa kushirikiana na Ofisi ya Mratibu Mkazi wa UN na Kikundi cha Mawasiliano cha UN, wamefanya uchambuzi wa miswada hiyo, wakiangazia uzingatiaji masuala ya kijinsia katika utungaji sheria.

Katika wasilisho lake, Hodan alisema ni lazima kuwapo uwiano wa 50:50 wa kijinsia katika michakato ya kisiasa.

Alisema lengo la mikataba hiyo ni kupata suluhisho la matatizo yanayowakumba wanawake wanaposhiriki katika siasa na uongozi ikiwamo kukuza na kulinda haki zao. "Kuna mikataba maalum ya kikanda na kimataifa inayolenga kukuza na kulinda haki za wanawake kama vile mikataba ya kimataifa ya kuondoa aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake ya mwaka 1979.

"Pia kuna Azimio la Beijing 1995, Sera ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2018 na Itifaki ya Jinsia na Maendeleo ya SADC," alisema. Hodan alisema mikataba hiyo pamoja na utafiti mbalimbali vinaonesha ushiriki finyu wa wanawake katika uongozi na ngazi ya uamuzi ni kikwazo katika kufikia maendeleo endelevu na huathiri jitihada za nchi kukuza demokrasia na uchumi.

Mratibu Mkazi wa UN nchini, Zlatan Milisic, alisema licha ya Tanzania kuwa na Rais wa kwanza mwanamke, bado iko nyuma ya makubaliano ya mkataba huo kwa kuwa wanawake ni asilimia 37 ya idadi ya wabunge waliopo bungeni; mahali mnamotungwa sheria na ni chombo kikubwa cha uamuzi.

Alisema licha ya kuwapo sheria zinazotambua umuhimu wa watu wote kushiriki katika uongozi na vyombo vya kufanya uamuzi, bado wanawake wanapitia changamoto zinazowarudisha kuwania nafasi hizo.

Alisema kwa kuona changamoto hizo waliunda kikosi kazi cha kuangazia masuala ya kidemokrasia kwa mwaka 2021-2022 na kilitoa mapendekezo ili kurejesha uwiano huo.

Mhadhiri wa Sheria kutoka Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT), Dk. Victoria Lihiru, alisema kikosi kazi hicho kilitoa mapendekezo katika maeneo tisa ikiwamo hitaji la kufanya mabadiliko katika sheria za uchaguzi na vyama vya siasa, umuhimu na hatua kupata katiba mpya pamoja na kuongeza ushiriki wa wanawake katika siasa.

"Kikosi kazi kinapendekeza umuhimu wa kuweka mikakati ya kupinga unyanyasaji dhidi ya wanawake katika siasa, vyama kuhakikisha asilimia 40 ya viongozi wake ni wanawake na kila chama cha siasa kuwa na sera ya jinsia," alisema.

Dk. Victoria aliongeza kuwa kikosi hicho pia kinapendekeza kuimarishwa mifumo ya ufuatiliaji ujumuishwaji wanawake na makundi maalum katika vyama vya siasa.

Miswada hiyo ilisomwa kwa mara ya kwanza bungeni Novemba mwaka jana. Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuanzia Januari 6-10, mwaka huu, ilipokea maoni kutoka kwa wadau mbalimbali vikiwamo vyama vya siasa, asasi za kiraia na viongozi wa dini.



Timu ya Kampeni ya Huduma ya Msaada wa kisheria ya Mama Samia ikishangilia baada ya kufanikiwa kuwaunganisha Temistocules Ijengo na Neema Joseph (walioshikana mikono), ambao walitengana katika ndoa yao kwa muda wa miaka mitatu na kusababisha watoto wao saba kuishi kwa kujitunza wenyewe. **Habari Uk. 8. PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Meli zafurika Bandari ya Dar

Na Mary Geofrey

MKURUGENZI wa Bandari ya Dar es Salaam, Mrisho Mrisho, amesema kuwapo ongezeko la meli zaidi ya 30 zinazosubiri foleni ya kushusha mizigo ni neema inayotokana na kuongezeka ufanisi kiutendaji katika bandari hiyo.

Amesema mafanikio hayo yametokana na kampeni ya kushawishi wateja wa nchi mbalimbali kushusha mizigo yao kupitia bandari hiyo na kuongeza ufanisi na utendaji kazi wa saa 24.

Mrisho alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu utendaji kazi wake.

Alisema kuwapo meli nyingi zinazosubiri kuingia kwenye gati ili kupakua mizigo ni kutokana na wateja wengi kuhamasika kupitisha mizigo ya Bandari ya Dar es Salaam na mizigo yake kusafirishwa kwa barabara kuelekea nchi jirani.

"Yapo magati 12 yanayofanya kazi na kwa sasa meli zipo 38 zinazopakua mizigo hapa Bandari ya Dar es Salaam na zimeanza kupungua hadi kesho kutwa tutakuwa tumemaliza meli 12.

"Kama ambavyo mmeshuhudia, watu wanafanya kazi kwa saa 24 hadi siku ya Jumapili kama leo (jana). Lengo ni kuhakikisha tunaendana na kasi ya mizigo tunayopokea. "Hatuwezi kusema tumeelemewa kwa sababu meli zinapakua na kuondoka na kesho (leo) tunatarajia kupokea meli nyingine kubwa 16 zinazoingia, ina maana zinaongezeka na kupungua, kazi kubwa inafanyika na nzuri," alisema.

Mrisho alisema dawa ya kupunguza msongamano huo ni kuongeza magati na maeneo ya kuhifadhia mizigo ili kuruhusu meli nyingi zaidi kuendelea kupewa huduma.

Mkurugenzi huyo alisema mafanikio hayo yamewahakikishia kuvuka lengo la kuhudumia shehena. Alisema mwaka wa fedha wa 2023/24 wamewekewa lengo la kuhudumia tani milioni 22 na tayari kwa kipindi cha nusu mwaka wameshahudumia tani milioni 12, hivyo kubakisha tani milioni 10 kutimiza lengo, lakini wana uhakika wa kuhudumia tani milioni 24.

"Haya malengo yanawekwa na wizara kwa kutumia wataalamu wa fedha kwenye Bunge la Bajeti, hatujiwekei wenyewe.

"Tunachofanya ni kupambana kufanya kazi usiku na mchana kuhudumia meli nyingi zaidi kadri tunavyoweza kwa ufanisi mkubwa ili kufikia lengo hili," alisema Mrisho.

Alisema kwa mwaka uliopita, bandari zote zilihudumia tani milioni 24, kazi ambayo wanatarajia itafanywa na Bandari ya Dar es Salaam peke yake ikiwa ni malengo binafsi waliyojiwekea.

Alisema mpango mkakati ni kuongeza eneo la Bandari Kavu ya Kwala ili wateja kuchukulia mizigo pale kwa urahisi kupunguza msongamano bandarini.

Mrisho alisema miradi ya kimkakati kama ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR) na ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) imekuwa chanjo cha ongezeko kubwa la mizigo inayoshushwa kwenye bandari na kuongeza ufanisi wake.

WORLD BANK GROUP

SALE OF USED VEHICLES TOYOTA LAND CRUISER PRADO TX

| Lot# | Make | Model | Year | Reg. Number |
|---|---|---|---|---|
| 01 | Toyota L/Cruiser Prado TX | 5L Diesel Engine | 2022 | T208CD182 |
| 02 | Toyota L/Cruiser Prado TX | 5L Diesel Engine | 2022 | T208CD183 |

Sealed bids are invited for purchase of the above vehicles. The vehicles are sold on "as is where is" basis

**Viewing:** The vehicle may be viewed from **Tuesday 16th to Thursday 18th January 2024** and from Monday 22nd to Thursday 25th January 2024 from 10:00 to 14.00 hours at World Bank Offices (Parking Lot), at Plot 50 Mirambo Street, Dar es Salaam.

**Contact Person:** Resource Management Officer

**Closing date:** **January 26th 2024 at 10:00 hours**

**Opening Bids:** All Bids will be opened in public on January 31st ,2024 at 11:30 hours in the World Bank, Conference Room on 1st floor, plot 50 Mirambo Street. All bidders or their authorized representatives must attend.

**Minimum Bid Price: For T208CD182 is Tsh. 84,675,319.00, T208CD183 is Tsh. 85,875,320.00**

**Terms of payment:** Currency: bids should be in either Tanzanian shillings or USD Dollar, but for comparison purpose, the offers in US$ WILL BE CONVERTED to Tanzania Shillings at the Bank of Tanzania exchange rate (selling) applicable one day before the submission date. Bids in any other currency will be rejected.

The successful Bidder will be required to pay a non-refundable cash deposit on the spot which is **25% (twenty-five percent)** of the offer. Full payment of the remaining amount must be deposited in the World Bank (IBRD) bank account within one week (five working days) from the date of submission of the bids. Failure to comply with this condition, will automatically nullify the sale without notice.

**Please Note:** The vehicle is exempted from duty. Successful bidder will be required to pay all Government taxes before being allowed to take the vehicle.

The Bids should be addressed to the Country Director, World Bank, P.O. Box 2054 Dar es Salaam, and should be sealed and clearly marked vehicle tendering as follows:
Lot # 01. T208CD182 or Lot no. 02. T208CD183 Toyota Land Cruiser Prado TX

**The bids should be deposited in the Tender Box at the World Bank Reception area, 5th Floor before the deadline for submission."The World Bank Office reserves the right to reject any or all Bids.**

## HABARI KITAIFA

# CCM yaibuka na lao kwa Mbowe, Lissu

**Na Beatrice Shayo**

SIKU moja baada ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kutangaza msimamo walioweka dhidi ya miswada ya sheria kuhusu masuala ya siasa na uchaguzi iliyowasilishwa bungeni, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimeibuka, kikikosoa msimamo huo.

Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, alitangaza hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari katika ofisi mpya za chama hicho, Mikocheni, Dar es Salaam, kuwa uamuzi huo unaoambatana na mpango wa kufanya maandamano, unatokana na maazimio ya kikao cha dharura cha Kamati Kuu kilichofanyika Januari 8, mwaka huu.

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Paul Makonda, katika kujibu hoja za CHADEMA jana, alisema mnufaika mkubwa wa maridhiano ambayo yamemfanya awe huru na kesi zake za kisiasa ni Mwenyekiti wa CHADEMA, Mbowe.

Makonda alitoa kauli hiyo ikiwa ni siku moja baada ya Mbowe kuzungumza na waandishi wa habari na kudai maridhiano yamekiukwa na kutangaza maandamano ya amani kuanzia Januari 24, mwaka huu kushinikiza miswada ya sheria kuhusu masuala ya siasa na uchaguzi iondolewe bungeni.

Makonda aliwaambia waandishi wa habari jijini jana kuwa ameshangazwa na kauli ya Mbowe dhidi ya Mwenyekiti wao wa CCM, Rais Samia Suluhu Hassan, wakati alinufaika na maridhiano.

"Tumepata nafasi ya kumsikia kaka yetu Freeman Mbowe akituhumu na kutoa kauli dhidi ya kiongozi wetu bila kujali dhamira njema aliyoonesha Mwenyekiti wetu wa CCM, Dk. Samia Suluhu Hassan," alisema.

Makonda alisema kuwa taifa kwa mara ya kwanza limeshuhudia haki ikisimamiwa kikamilifu ikiwa ni jitihada binafsi za Mwenyekiti wao wa CCM alizozifanya katika kuunda Tume ya Haki Jinai kupitia mambo kadhaa ili kuhakikisha Mtanzania anapata haki yake bila kujali rika, elimu, kipato, kabila, dini na hata kule alikotoka.

"Mbowe kaeleza maneno mazito sana, upo wakati tumetafakari ya kwamba hakuna sababu ya kumjibu, lakini imefika wakati tukasema hapana! Kwanini tumwache apotoshe umma kwa kichocheo ambacho hatuelewi msingi wake ni nini?" Makonda alidai.

Alisema moja ya hoja kubwa aliyosimama nayo katika mchakato huo wa miswaada wa sheria (Sheria ya Vyama vya Siasa, Tume ya Uchaguzi na Sheria ya Uchaguzi yenyewe), amediriki kusema hadharani ya kwamba mapendekezo yaliyotolewa na kikosi kazi kilichoundwa na Rais pamoja na yaliyotolewa na wadau mbalimbali yamepuuzwa, jambo ambalo kwao CCM wanaona si la kweli.

"Mbowe anafahamu katika mapendekezo 84 yaliyotolewa, mapendekezo 63 yote yamechukuliwa na yapo kwenye muswada ambao hatua za kisheria zinaendelea katika kuunda kwa sheria na yeye ni mnufaika mkubwa wa maridhiano ambayo yamemfanya akawa huru na kesi zote za kisiasa.

"Kuachiwa huru bila masharti na yeye mwenyewe na chama chake na vingine kufanya mikutano ya hadhara bila kubugudhiwa tena kwa ulinzi mkali chini ya Jeshi la Polisi kuhakikisha dhamira ya Rais Samia inatimia si tu kwa vyama vya siasa bali kwa Watanzania wote," alisema.

Makonda alisema kuwa kabla ya Mbowe kwenda barabarani kufanya maandamano, wafanye mdahalo wa wazi utakaomjumuisha Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu na Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika.

"Wito wangu kwa Mbowe kabla ya kwenda barabarani na wala hatusemi kwamba usiende, ziko mamlaka zinazohusu utaratibu wa namna gani uweze kuandamana na kwa sababu Rais wetu anasimamia 4R na kuzingatia sana ujenzi wa demokrasia na msingi wake ni maridhiano, ninakuomba Mbowe, Mnyika na Tundu Lissu kabla hamjawapeleka Watanzania barabarani, mimi kama Mwenezi wa CCM Taifa niko tayari tufanye mdahalo wa wazi ambao ningetamani uandaliwe na wanahabari na ikipendeza Mbowe uchague wanahabari unaowataka watakaoandaa mdahalo huu.

"Nitapenda uje na timu yako, mimi nitakuja peke yangu ili ueleze yale ambayo unakusudia kuwapeleka Watanzania barabarani na mimi niyaseme yetu ili sasa Watanzania wachague kwenda barabarani kuvuruga uchumi wa taifa lao au kubaki kujenga maridhiano na umoja wa kitaifa chini ya Rais Samia," alisema.

Makonda alisema wanafahamu Mbowe yupo kwenye wakati wa uchaguzi ndani ya chama chake, akidai hali ya kisiasa ndani ya chama chake si aliyotarajia. Alisema CCM wanamshauri aridhie demokrasia ndani ya chama, kama wanachama wanataka kumchagua mwengine awe mwenyekiti wao badala yake.

"Kupeleka watu kuandamana si sawa, viongozi wote wa kisiasa na wa dini waliotoa maoni yao, ni sawa na kupuuzia... mtu yeyote anayetaka utawala bora na amani atakaa kwenye meza ya majadiliano," alisema Makonda.

Alidai dhamira ya Mbowe si njema na siku zote ni kutaka kumkatisha tamaa Rais na hata Watanzania wanaopenda maendeleo.

"Kila unapoanzishwa mchakato wa kuleta maendeleo, Mbowe anakuwa wa kwanza kuvuruga mchakato huo, mtakumbuka tuliingia kwenye mchakato wa katiba kubadilisha baadhi ya vifungu vya sheria, lakini Mbowe na wenzake walikataa, wakasema wanataka Katiba Mpya kwa maana katiba yote haina maana," alidai.

"Alikimbia Bunge la Katiba na kuanzisha vuguvugu huko mtaani, kila alichosema Mbowe, Rais Samia aliridhia na wakati mwingine alikubali kukinzana na wana CCM wenzake ili kujenga mustakabali mpana wa taifa moja lisilobaguana na vyama, lakini matokeo yake jana (juzi) Mbowe katangaza tena kuacha mchakato huu wenye dhamira njema na kukimbia mtaani kuhamasisha maandamano," alisema Makonda.

Katika hoja zake juzi, mbali na mambo mengine, Mbowe alisema Kamati Kuu ya CHADEA imetathmini na kujiridhisha kwamba serikali haitaki kuwapo maboresho ya msingi katika mfumo wa uendeshaji wa uchaguzi nchini na ukuaji wa demokrasia.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya GEITA Kituo cha NYANKUMBU Mkoa wa GEITA**
**Shauri la Ndoa Na...47..2023**
**Jina la Mdai ELIZABERTH PETER**
**Jina la Mdaiwa MAICO EDWARD**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Kwa MAICO EDWARD SENGEREMA**
**Kwa kuwa mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba.. YA TALAKA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 23 Mwezi 1 Mwaka 2024 saa 8:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 14 Mwezi 12 Mwaka 2023

HAKIMU
RESIDENT MAGISTRATE
GEITA

..............................
**HAKIMU**

---



UCB
CARING FOR FAMILY ECONOMY

## UCHUMI COMMERCIAL BANK LTD

### UONESHAJI WA GHARAMA TAREHE 31 DISEMBA 2023

| B | DEPOSIT RATES | | RATES |
|---|---|---|---|
| | Savings Account **(p.a)** | | 1% |
| | Mavuno Account - Special Deposit Account (p.a) | | 9% |
| | **Fixed Deposit** | | |
| | 3 Months | | 4% |
| | 6months | | 5% |
| | 12Months | | 6% |
| | Negotiable rates for Amount Exceeding 50Mil | | 6% to 7% |
| | Negotiable rates for Amount Exceeding 100Mil | | 8% to 9% |
| | Negotiable rates for Amount Exceeding 500Mil | | 10% |
| C | **CHARGES AND FEES** | | |
| | **ITEM/TRANSACTION** | | **CHARGE/FEE** |
| 1 | **Current Accounts** | **USD** | |
| | Minimum Opening balance - Company and individual | 50.00 | 100,000.00 |
| | Monthly Statement enquiry | 2.00 | TZS 1,500 per month and TZS 700 for extra page |
| | Monthly Ledger fee | 10.00 | 15,000.00 |
| | Account closing charges | 10.00 | 20,000.00 |
| | Sale of bankers cheque | | 30,000.00 |
| | Cancelation of bankers cheque | | 30,000.00 |
| | Cheque book per leaf | 0.18 | 400.00 |
| | Stop payment order | 10.00 | 30,000 reported lost/stolen cheque book/leaf (per notice) |
| | Standing order within the bank per entry | 2.00 | 2,000.00 |
| | Standing order to other banks per entry | 20.00 | 15,000.00 |
| | Confirmation of Balance and Audit statement | 25.00 | 50,000.00 |
| | Salary processing fee per entry | N/A | 2,000.00 |
| | Upaid cheque (RD) | 40.00 | 40,000.00 |
| | Montly fees - Parishes Account | N/A | 5,000.00 |
| | - Other Current Account | N/A | 15,000.00 |
| | Quartely fees - Other Current account | | 2,000.00 |
| | Deposit fee | N/A | free |
| | Withdrawal on current account using cheque | | Up to TZS 400,000 TZS 1,500, 400,000.001 to 5,000,000 TZS 2,000 from 5,000,000.001 above 0.05% max 150,000 |
| 2 | **Savings Accounts** | | |
| | Minimum Operating Balance | Mavuno Saving Account | 5,000.00 |
| | | Uchumi Account | 10,000.00 |
| | | Personal Saving | 20,000.00 |
| | Account closure | | 20,000.00 |
| | Dormant account reactivation | | free |
| | Withdrawal fee over the counter | 1% of the amount | Up to TZS 400,000 TZS 1,500, from 400,000.001 to 5,000,000, from 5,000,000.001 to 10,000,000 TZS 2,000 from 10,000,000.001 to 50,000,000 TZS 10,000,000 from 50,000,000 TZS 0.05% max TZS 150,000 |
| | Account maintenance fee - Monthly | | 1,500.00 |
| | - Quartely | | 1,600.00 |
| | Bulk Cash deposit | | free |
| | New ATM card issuance | N/A | 10,000.00 |
| | ATM card renewal or replacement | N/A | 15,000.00 |
| | ATM withdrawal fee | | 1,300.00 |
| | PIN Reset ATM | | 5,000.00 |
| 3 | **Electronic Banking** | | |
| | SWIFT/TISS transfer | | 11,800.00 |
| | Mobile banking balance enquiry | | 200.00 |
| | Transfer from bank account to mobile | | |
| | Mobile - PIN reset | | 2,000.00 |
| | **Other Charges** | | |
| | Cheque clearing fee (Outward Cheques) | | 1,000.00 |
| | EFT | | 2,000.00 |
| | Search fees (including vouchers) | | one month free, 2 to 6 months 20,000, above 6months 50,000. CCTV footage 30,000 max 6months |
| | Uncollected cheque book (after notification) | | TZS 2,000 per month |
| | Coins deposit | | 3% of the deposited amount (non parish) |
| | Brela Search Fees | Company Limited | TZS 25,000 |
| | | Trade name | TZS 7,000 |
| 4 | **Internet Banking** | | |
| | 24/7 Transfer UCB to UCB | | Free |
| | 24/7 Transfer (Other Banks) | | 11,800.00 |
| | 24/7 Fund transfer (Bank to Mobile) | Tzsh 1,000 -100,000 | 2,000.00 |
| | 24/7 Fund transfer (Bank to Mobile) | Tzsh 101,000-200,000 | 3,000.00 |
| | 24/7 Fund transfer (Bank to Mobile) | Tzsh 201,000-500,000 | 5,000.00 |
| | 24/7 Fund transfer (Bank to Mobile) | Tzsh 500,1000-1,000,000 | 6,000.00 |
| | 24/7 Fund transfer (Bank to Mobile) | Tzsh 1,001,000-2,000,000 | 8,500.00 |
| | 24/7 Airtime processing | Payment | free |
| | 24/7 Government payment | | free |
| | 24/7 Other payments (utility) | DSTV, Star Times, AZAM, Water Bills etc. | 1,500.00 |
| | Balance inquiry | | Free |
| | Monthly fee per retail user | | 1,500.00 |
| | Monthly fee for corporate user | | 2,500.00 |
| | Retail & Corporate subsricption | | Free |
| | Bank statement self download | | 500.00 |
| | Cheque book request 100 leaves | | 47,200.00 |
| | Cheque book request 50 leaves | | 23,600.00 |
| | PIN Regeneration | | Free |
| | Salary processing | | 1,800.00 |
| | Standing Order Instructions | | 2,000.00 |

Air Tanzania
Training Centre



**KOZI YA WAFANYAKAZI NDANI YA NDEGE (CABIN CREW).**

Chuo Cha Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL Training Center ) kina furaha kuwatangazia watanzania wote kuwa kwa mara nyingine kitaendesha kozi ya wafanyakazi ndani ya ndege (Cabin Crew ) kuanzia tarehe 01 Machi 2024. Kozi hii ni ya muda wa miezi mitatu (03), chuo kipo uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere-Dar es salaam(JNIA) Terminal One kwenye jengo la utawala la ATCL karibu kabisa na kituo cha polisi uwanja wa ndege. Chuo kinakaribisha maombi ya kujiunga na kozi hii kwa wenye sifa zilizoainishwahapo chini. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 31 Januari 2024

**Sifa za mwombaji.**

i. Awe na umri kuanzia miaka 18 hadi miaka 25
ii. Muomaji asiwe na michoro yoyote ya kudumu inayoonekana mwilini (visible tattoo)
iii. Awe timamu kiakili, kimaumbile na urefu kuanzia futi 5"4 (162 cms) na kuendelea
iv. Elimu sio chini ya kidato cha nne na kufaulu angalao masomo manne, hasa masomo ya Kiingereza na Jiografia
v. Aweze kuongea na kuandika kwa ufasaha lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Muombaji mwenye uelewa wa lugha zaidi ya hizi mbili kama Kiarabu, Kichina, Kihindi na Kifaransa atapewa kipaumbele.
vi. Awe Mtanzania au raia wa kigeni mwenye vibali halali vinavyomruhusu kukaa na kusoma nchini.

**Angalizo:** Waombaji kutoka nchi za kigeni watatakiwa kulinganisha matokeo ya vyeti vyao kwenye Baraza la Mitihani Tanzania (NACTE) yafanane na matokeo ya Tanzania.

**Barua ya maombi iambatane na vitu vifuatavyo.**

i. Nakala ya cheti cha kidato cha nne na vyeti vingine vya shule/chuo alikosoma
ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
iii. Picha mbili ndogo (passport size) na picha moja yenye kuonyesha umbo lote ukubwa wa 6x8
iv. Curriculum Vitae –CV

**Maombi yatumwe kwa:**
**Mkuu wa Chuo,**
**ATCL Training Center**
**Box no 543**
**Dar Es Salaam**
**Email, training@airtanzania.co.tz**

**Kwa mawasiliano zaidi, tafadhali piga namba hizi TU:**
**Mob: +255754 345 874, +255735 787212**

**ATCL TRAINING CENTER**
**"FULFILL YOUR FLYING DREAMS WITH US"**

# Mtambo Bwawa la Nyerere kuwashwa kesho

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Umeme (TANESCO) limetangaza kesho kuwashwa kwa mtambo mmoja wa kuzalisha umeme wa megawati 235 kutoka kwenye Bwawa la kufua umeme la Julius Nyerere (JNHPP) na kuingizwa kwenye gridi ya taifa.

Shirika hilo limesema limeshaanza awamu ya pili ya maandalizi ya kupokea umeme kutoka JNHPP kwa kuunganisha kituo kipya cha kupoza umeme wa 400kV Chalinze na njia ya Msongo wa Kilovoti 220 inayoanzia Luguruni hadi mkoani Morogoro.

Akizungumza kwenye eneo la mradi, Mhandisi Newton Livingstone ambaye ni Meneja Mradi Kituo cha Chalinze, alisema Jumamosi walikata njia ya umeme ya kutoka Morogoro kwenda kituo cha Luguruni kama sehemu ya maandalizi.

"Haya ni maandalizi ya kupokea umeme wote utakaoanza kuzalishwa na JNHPP kuanzia tarehe 16 mpaka tarehe 19 kwa hiyo tumeona tujizatiti kwa mifumo na hii ni awamu ya pili zile Megawati 235 za mashine zinazoenda kufanyiwa majaribio zitakuwa na uwezo wa kuingizwa kwenye gridi ya taifa kupitia ile njia ambayo tuliikata mwezi Desemba na njia hii ambayo tuliikata Jumamosi," alisema.

Kwenye taarifa yake kwa vyombo vya habari mwishoni mwa wiki, shirika hilo lilisema limeanza awamu ya pili ya maandalizi ya kupokea umeme kutoka kwenye mitambo ya kufua umeme ya bwawa la Nyerere kuuingiza kwenye gridi ya taifa.

Kwa mujibu wa taarifa ya shirika hilo, maandalizi hayo ni ya kuunganisha kituo kipya cha kupoza umeme wa 400kV Chalinze na njia ya Msongo wa Kilovoti 220 inayoanzia Luguruni hadi mkoani Morogoro.

Ilisema kazi hiyo itakapokamilika itaongeza uwezo wa Kituo cha 400kV Chalinze kupokea umeme utakaozalishwa kwenye mitambo ya Bwawa la Julius Nyerere na kuingizwa kwenye gridi ya taifa.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, kazi hiyo ilianza Jumamosi (Januari 13) na inatarajiwa kukamilika Januari 21 na kwa kipindi ambapo kazi inaendelea kutakuwa na athari za kutopatikana kwa umeme kwa nyakati tofauti.

Ilisema maeneo yatakayoathirika ni yaliyounganishwa na gridi ya taifa kwasababu njia ya msongo wa kilovolti 220 kutoka Luguruni kwenda Morogoro itazimwa na kuingia kwenye kituo cha kilovolti 400 Chalinze.

"Kuzimwa kwa njia hii kutaathiri uwezo wa usafirishaji wa umeme kwenda mikoani na ubora wa umeme kwa mikoa ya Pwani na Dar es Salaam na kwasababu hizi shirika litalazimika kupunguza matumizi ya umeme kwa wateja ili kuendana na uwezo wa njia za usafirishaji na kuwa na uhakika wa ubora wa umeme," ilisema.

Taarifa hiyo ilisema kuhamishwa kwa njia hiyo kwenye kituo cha kupoza umeme cha Chalinze na njia zingine za usafirishaji umeme zitakazohamishiwa kwenye kituo hicho siku za karibuni kutasaidia kusafirisha umeme unaozalishwa kwenye bwawa la JNHPP.

Ilisema umeme huo utasafirishwa kupelekwa kwenye maeneo mbalimbali ya nchi ili kuongeza kiwango cha umeme hali ambayo itaondoa shida ya nishati hiyo nchini.

Bwawa la JNHPP lina mitambo tisa ambayo kila mmoja utakuwa na uwezo wa kuzalisha Megawati 235 na kwa ujumla wake itakapoanza uzalishaji itazalisha Megawati 2,115 za umeme na kuondoa tatizo la umeme kwenye maeneo yote nchini.

Ujenzi wa bwawa hilo ambalo liko kwenye hatua za mwisho unafanywa na moja ya kampuni kubwa ya ujenzi Afrika ya Kati na Afrika Arab kutoka Misri kwa ushirikiano na Elsewedy.

Ujenzi wa mradi huo ambao kwa sasa umevuka asilimia 92 ulianza kutekelezwa mwaka 2018 baada ya kampuni hiyo kusaini mkataba na serikali wa kuukamilisha mradi huo kwa miezi 42 lakini umekuwa ukichelewa kukamilika kwa wakati kutokana na sababu mbalimbali.

# Sababu kupaa bei ya nondo, misumari

**Na Halfani Chusi**

NAIBU Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, amesema kupanda kwa bei ya nondo na misumari kumetokana na uhaba wa chuma ghafi na chakavu ambavyo ndio malighafi inayotumika kutengenezea bidhaa hizo.

Kigahe alibainisha hayo jana alipozungumza na mwandishi wa habari hizi aliyehoji sababu za kupanda kwa bei ya bidhaa hizo.

Naibu Waziri huyo alisema kupanda kwa bei kunategemeana na soko la chuma duniani, akiwa na ufafanuzi kwamba viwanda vingi kwa sasa vinategemea chuma ghafi toka nje ya nchi.

"Bei hizi ni za kimataifa, ndio maana unaona bei inaongezeka, ndio maana tumeruhusu hata chuma chakavu kutoka nje kuuzwa hapa (nchini) ili kusaidia (kukabili) huo upungufu.

"Tunajitahidi kutoa taarifa sahihi kwa wakati kwamba kuna changamoto hizo na mpango wa serikali ni upi katika kuhakikisha bei inashuka. "Tunachokifanya sasa ni kupata wawekezaji kuzalisha chuma ghafi, kwa sababu chuma kinapotoka nje ya nchi, kinakuja kwa gharama zinazosababisha ongezeko kwa mlaji wa mwisho," alifafanua.

Naibu Waziri Kigahe alitaja jambo lingine linalochangia kupanda kwa bei ya bidhaa hiyo kuwa ni mahitaji ya soko kwa walaji; wauzaji wengi wanaangalia namna walivyoipata bidhaa hiyo na wauzaje ili wapate faida.

Kiongozi huyo pia aliwataka Watanzania kujenga utamaduni wa kununua bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani ili kuchochea ukuaji wa uchumi.

"Wenye viwanda pia wanatakiwa kuzalisha bidhaa bora na zenye bei rafiki, kama hazitakuwa na ubora tutashindwa kushindana na zile za kutoka nchi jirani.

"Hatari ninayoiona kama wakiendelea kuzalisha bidhaa zisizo na ubora, wateja watakimbilia zile za kutoka nje ya nchi, hali itakuwa mbaya sana kwa ustawi wa nchi na viwanda," alihadharisha.

Kumekuwa na malalamiko toka kwa wananchi kwamba bei ya nondo na misumari imepanda katika maeneo yao, baadhi wakidai kuna ongezeko la Sh. 2,000 katika kila nondo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kongole waamuzi Mapinduzi Cup, Ligi Kuu Bara wajifunze

**MICHUANO** ya Kombe la Mapinduzi visiwani Zanzibar imemalizika kwa timu ya Mlandege FC kutwaa ubingwa baada ya kuifunga Simba kwa bao 1-0 kwenye mchezo wa fainali uliopigwa Jumamosi iliyopita katika Uwanja wa New Amaan Sports Complex, ukihudhuriwa na mashabiki kibao.

Timu hizo, zote zilifika fainali kwa mikwaju ya penalti baada ya matokeo ya dakika 90 kuwa sare, Mlandege ikitoka suluhu na APR ya Rwanda na Simba ikitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Singida Fountain Gate FC na kisha changamoto ya mikwaju ya penalti ikazivusha.

Katika michuano hiyo tangu imeanza hadi mwisho, licha ya kuwapo kwa changamoto mbalimbali, lakini lipo la kujifunza kwa waamuzi wa Ligi Kuu Tanzania Bara kutoka kwa waamuzi waliochezesha mechi hizo za Kombe la Mapinduzi.

Kwa waliofuatilia michuano hiyo kwa umakini mwanzo mwisho watakubaliana nasi kwamba palikiwapo na makosa kadhaa yaliyofanywa na waamuzi, ambayo kwetu sisi tunayachukulia kama ya kibinadamu na ndiyo maana kwa wenzetu walioendelea kisoka duniani, wamefikia hatua ya kuweka Teknolojia ya Video ya Kumsaidia Mwamuzi, VAR.

Hata hivyo, pamoja na mapungufu yaliyojitokea, hatuna budi kuwasifu kwa upande wakuhakikisha mpira unachezwa kwa dakika zote 90 kwa kuufidia ipasavyo muda wote unaopotezwa na wachezaji ama kwa makusudi au wanapoumia na mambo mengine kama hayo yanayosabisha mpira kusimama.

Wapo ambao kwa kutojua kwao walikuwa wanatafsiri kwamba waamuzi walikuwa wakizibeba baadhi ya timu hasa wakati wanapoongeza dakika sita hadi saba za majeruhi halafu mwamuzi akazidisha mpira ukachezwa kwa dakika tisa ama 10 na zaidi.

Katika hilo, tunaungana nao na kuwapo kongole, lakini pia tukiwataka mashabiki wa soka nchini kutambua kwamba mwamuzi wa akiba anapoinua ubao kuonesha dakika za nyongeza ni tano ama saba haruhusiwi tena baadaye kunyanyuka na kuongeza nyingine endapo muda alioongeza hukutumika ipasavyo kwa mpira kuchezwa.

Jukumu hilo hubaki kwa mtunza muda mkuu uwanjani, yaani mwamuzi wa kati, ndiye anapaswa kuufidia kwa kuongeza muda hata kama ule uliooneshwa na mwamuzi wa akiba umemalizika.

Wengi wanachokikosea wakiwamo mashabiki wa soka, wachezaji na hata baadhi ya waamuzi ni kudhani muda ule wa nyongeza ukishamalizika refa anatakiwa kumaliza mpira bila kujali mpira ulitumika ipasavyo kwa mpira kuchezwa.


Tunaelewa na tumekuwa tukishuhudia baadhi ya wachezaji wamekuwa wakiutumia muda wa nyongeza kwa kujiangusha kuonyesha wamechezewa madhambi au kuchelewa kutoka pale kocha anapofanya mabadiliko, jambo ambalo humlazimu mwamuzi kuongeza muda zaidi baada ya ule wa nyongeza kumalizika.

Katika hilo, hatuna budi kuwaelimisha wote wasiojua hususan ni kwa baadhi ya wachezaji, kwamba kinachotakiwa kufanya ili kutoongezwa tena muda baada ya uleo wa nyongeza kumalizika, ni kuumiliki mchezo hasa kwa kucheza pasi ili na si kutoa mpira nje ama kujiangusha angusha.

Kwa ujumla waamuzi Kombe la Mapinduzi waliutendea haki kuhakikisha mpira unachezwa kwa dakika zote 90, jambo ambalo linapaswa kuwa somo pia kwa waamuzi wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambao mara nyingi hata timu ipoteze muda kiasi gani ni nadra kuona zimeongezwa tu dakika sita ama saba.

Lakini hata zikiongezwa zitakapomalizika mpira unaishia hapo hapo bila kujali kwamba zilizoongezwa zilitumika ipasavyo kwa mpira kuchezwa ama kwa ujanja ujanja wa wachezaji kujiangusha angusha ama kupoteza muda kwa njia nyingine.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wachezaji Zanzibar wameanza kulikamata soko la usajili Bara

Na Adam Fungamwango

**INAWEZEKANA** kwa mara ya kwanza katika historia ya soka la Tanzania, mwaka huu kukawa na idadi kubwa ya wachezaji waliosajili kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara kutoka Zanzibar baada ya michuano ya Kombe la Mapinduzi kumalizika Jumamosi iliyopita.

Kwa miaka takribani mitatu au minne hivi, timu za Bara zimekuwa zikiwasajili wachezaji kutoka Zanzibar mara tu baada ya kuwaona katika michezo ya Kombe la Mapinduzi.

Huko nyuma tuliona kina Hussein Abel aliyekuwa kipa bora mwaka 2021 kwenye michuano hiyo akiichezea timu ya Taifa Jang'ombe na baada ya hapo akatwaliwa, akavuka maji kuichezea Prisons, baadaye KMC na sasa yupo kikosi cha Simba.

Kipa Ibrahim Abdallah, yeye alikuwa akiidakia KVZ na sasa ni tegemeo kwenye kikosi cha Singida Fountaine Gate, Bashima Saul Saite ambaye msimu uliopita alikuwa Mlandege iliyotwaa ubingwa sasa yupo Geita Gold.

Januari 2022, Yanga ilimsajili beki Ibrahim Hamad 'Bacca' kutoka KMKM na kwa sasa si tegemeo kwa Yanga pekee bali hata kwa kikosi cha Timu ya Taifa, Taifa Stars.

Msimu huu ndiyo umetia fora, ukiacha Yanga iliyomsajili Shekhan Hamisi kabla ya michuano ya Mapinduzi, Simba imemsajili Seleh Karabaka kutoka JKU, KMC ikikamilisha usajili wa Abdallah Said Lanso kutoka Mlandege na straika wa KVZ, Akram Muhima.

Huu ni usajili tu ambao umekamilika, lakini kuna tetesi nyingi zinazowahusu wachezaji wa Zanzibar ambao wanatakiwa na timu mbalimbali za Bara.

Baadhi ya wachezaji wanaotajwa kuwa wataondoka Zanzibar kujiunga na klabu za Bara ni golikipa wa Mlandege aliyedaka mechi ya fainali juzi, Othmani Hassan ambaye inasekana KMC inakamilisha utaratibu wa kumsajili, golikipa wa JKU, Yacoub Suleiman anayetajwa kutakiwa na JKT.

Na sio hao tu, tunaweza kushuhudia na wengine pia. Hii inaonesha kuwa Zanzibar imeshaanza kuwa kitalu cha timu za Tanzania Bara.

Nina uhakika, ikiendelea hivi kwa misimu mitatu tu, basi Ligi ya Tanzania Bara inaweza kuwa na wachezaji wengi kutokea Zanzibar kuliko Bara.

Tangu enzi na enzi, kiuhalisia ni kwamba wachezaji wa Zanzibar wana ufundi zaidi miguuni kuliko wa Bara, lakini kilichokuwa kinawashinda wengi ukiondoa kina Innocent Haule, Thuwein Ally, Nadir Haroub 'Cannavaro', Abdi Kassim, Mohamed Nassor 'Chollo', Feisal Salum baadhi ya wachache ni nguvu.

Inaonekana kwa sasa walimu wanaowafundisha vijana Zanzibar wameshatambua udhaifu uliokuwa unawakwaza, na sasa ukiwaangalia wachezaji wa huko, pamoja na ufundi walionao, hivi sasa wana fiziki zaidi kuliko hata wachezaji wa Bara.

Pili kujituma kwao haijawahi kuwa tatizo, siku zote unapoangalia mechi yoyote anapokuwa mchezaji kutoka Zanzibar, kitu ambacho utakigundua ni upambanaji zaidi ukiwatofautisha na Bara.

Cannavaro, Chollo, Fei Toto, Bacca, ni sehemu ndogo tu ya mfano wa utofauti kati ya wachezaji wa Bara na Zanzibar.

Kingine ni kwamba wachezaji wengi wa Zanzibar wamekuwa na mwendelezo wa viwango vyao mechi hadi mechi na wanacheza kwa muda mrefu zaidi.

Na hii ni kutokana na kuwa na nidhamu hasa nje ya uwanja, mara nyingi hawana mambo mengi yanayosababisha viwango vya kuyumba yumba.

Hii ni kengele ya hatari kwa baadhi ya wachezaji wa Tanzania Bara, inabidi sasa wajiangalie wanakwama wapi.

Kwanza wengi wao wanataka pesa nyingi za usajili, lakini wanashindwa kujituma uwanjani, hawana mwendelezo wa viwango mechi hadi mechi, na wana mambo mengi nje ya uwanja.

Itafika wakati sasa si dirisha dogo tu wakati wa Kombe la Mapinduzi, bali hata msimu mpya wa usajili, klabu za Bara zitakuwa zikikimbizana Zanzibar kusaka wachezaji na kuwaacha wa Bara wakihaha.

Soko sasa litakuwa ni wachezaji kutoka nje, na wa hapa nchini nadhani kuelekea msimu ujao wachezaji kutoka Zanzibar watakuwa wanahitajika sana Bara.

Kwanza klabu zitakuwa zinapata wachezaji kwa pesa ndogo, halafu ni wachezaji mafundi na wapambanaji.

Na hili limeanza kuonekana kwenye Kombe la Mapinduzi mwaka huu. Dalili ya mvua ni mawingu, wachezaji wa Bara wabadilike, wasiseme sikuwaambia.

HABARI KITAIFA

# WMA, ZAWEMA zatia saini mkataba kushirikiana

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Vipimo Tanzania Bara (WMA) na Wakala wa Vipimo Zanzibar (ZAWEMA), umetia saini hati ya makubaliano ya ushirikiano (MoU) ili kuimarisha utendaji kazi wao katika maeneo mbalimbali.

Maeneo watakayoshirikiana ni kubadilishana utaalamu na vitendea kazi ili kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi wanaowahudumia kwa upande wa Bara na Visiwani Zanzibar.

Akizungumza baada ya kushuhudia utiaji saini huo, kituo cha maonesho ya biashara Nyamanzi Fumba, Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara Serikali ya Zanzibar, Dk. Hashil Abdallah, alisema ni vyema kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi hizo ili kuhakikisha vipimo vyote vinakuwa sahihi na mnunuzi wa bidhaa anapata kulingana na thamani ya fedha anayotoa.

Dk. Hashil alisema, kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo, wakala wa vipimo ndiyo taasisi pekee inayopaswa kusimamia matumizi sahihi ya vipimo kwa kuhakikisha kuwa vipimo vinavyotumika katika biashara viko sahihi na kuzingatia matumizi sahihi ili kuepusha madhara ili kulinda walaji. Aidha, alisema makubaliano hayo yatasaidia kuimarisha utendaji kazi na kuongeza ufanisi utakaosaidia kufikia malengo ya taasisi hizo kwasababu WMA ilianzishwa muda mrefu na ina uzoefu wa kutosha na vifaa vingi vya kisasa.

Alisema kwa ushirikiano huo, WMA itaiwezesha zaidi ZAWEMA kutumia pia vifaa hivyo na wataalamu ili kusimamia matumizi sahihi ya vipimo katika sekta nyingi zaidi.

Katibu Mkuu Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar, Ali Khamis Juma, alisema ushirikiano baina ya taasisi za WMA na ZAWEMA ni wa kudumu na utaisadia kukua zaidi na kuingia katika maeneo mengi ya kiutendaji kama ilivyo upande wa WMA Tanzania Bara.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Stella Kahwa, alisema ushirikiano huo umekuwapo muda ingawa haukuwa rasmi kimaandishi.

Alisema mara nyingi WMA na ZAWEMA hushirikiana kuendesha kaguzi mbalimbali visiwani Zanzibar kwa wauzaji wa vito na madini, mafuta na hata katika sekta ya gesi ili kuhakikisha vipimo vinakuwa sahihi wateja hawaibiwi.

Mkurugenzi wa ZAWEMA, Mohammed Simai Mwalim, alisema vipimo vikisimamiwa kwa usahihi katika bidhaa mbalimbali zinazozalishwa nchini na zinazoingizwa kutoka nje ya nchi itasaidia serikali kukusanya kodi kwa usahihi.

Alitoa wito kwa wananchi na wafanyabiashara wote wa Tanzania Bara na Zanzibar kutumia vipimo sahihi na wakikutana na changamoto yoyote inayohusu vipimo wafike kwenye ofisi za Wakala wa Vipimo kwa ajili ya kupata msaada wa kitaalamu.

Aliwaonya wafanyabiashara kutochezea vipimo ili kuwaibia wananchi, kwa kuwa ni kosa kisheria na hatua kali zitachukuliwa dhidi ya wote watakaobainika kufanya vitendo hivyo ambavyo vinakatazwa hata kwenye maandiko matakatifu.

Hati ya makubaliano ya kiutendaji ilisainiwa na Mtendaji Mkuu wa WMA, Stela Kahwa na kwa upande wa Zanzibar Mkurugenzi wa ZAWEMA, Mohammed Mwalim Simai.

# Kanisa KKKT lawakumbuka wajane kwa kuwapa mtaji

**Na Steven William,**
MUHEZA

KANISA la KKKT Usharika wa Muheza, limeamua kuwapa mtaji wajane ili waweze kufanya biashara mbalimbali za kustawisha uchumi wa familia zao.

Kadhalika kanisa hilo limeikumbusha jamii kuwajali wajane ikiwa ni njia mojawapo ya agizo la Mungu.

Wito huo ulitolewa jana na Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la KKKT Usharika wa Muheza mjini mkoani Tanga, John Ndimbo katika ibada ya Jumapili.

Ndimbo ameikumbusha jamii kukemea vitendo viovu ikiwamo udhalilishaji na ukatili wa kijinsia kwa wajane kwa kuwa hawakupenda kuwa katika hali hiyo.

Alisema kanisa hilo limeamua kuwakusanya wajane na kuwapa Shilingi milioni nne zitakazowasaidia kuanzisha mradi wa kukodisha maturubai na viti.

Alisema mwaka huu mpya wa 2024 kanisa lina ndoto kubwa ya kuanzisha miradi ikiwamo kujenga vibanda vya biashara kuzunguka kanisa na nyumba ya mchungaji eneo la Michungwani, Muheza.

Pia kanisa limeanzisha kitengo cha mwaka wa wanaume Dayosisi ya Kaskazini Mashariki ambacho kitakuwa na miradi mbalimbali ya maendeleo.

Katibu wa kitengo hicho cha mwaka wa wanaume Jackson Saria, alisema wamepanga kuanzisha mradi wa shule kuanzia darasa la awali pamoja na kununua vyombo vya muziki kwa ajili ya kwaya ya wanaume.

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa Kamati ya fedha katika kanisa hilo, Bright Mshana, alitoa mchanganuo wa mapato na matumizi mbalimbali ya bajeti katika kuendeleza miradi mbalimbali.


MWANGA HAKIKABANK

## MWANGA HAKIKA BANK LIMITED
## MINIMUM DICLOSURE OF CHARGES AND TARIFFS

| PRODUCTS/ SERVICES | BUSINESS CURRENT A/C | PREMIUM CURRENT A/C | PERSONAL SAVING A/C | SALARY A/C | MTOTO SAVING A/C | JIPANGE SAVING A/C | WEKEZA GROUP A/C | MALENGO SAVING A/C | FOREX ACCOUNT USD & EURO | JIWEKEE SAVING A/C | MHB PAMOJA A/C | MSOMI ACCOUNT |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Account opening | 100,000.00 | 50,000.00 | 20,000.00 | 0 | 10,000.00 | 10,000.00 | 20,000.00 | 100,000.00 | 10 | 0 | 50,000.00 | 10,000.00 |
| Minimum operating Balance | 100,000.00 | 50,000.00 | 10,000.00 | 5,000.00 | 5,000.00 | 0 | 10,000.00 | 100,000.00 | 10 | 10,000.00 | 50,000.00 | 5,000.00 |
| Interest Payable | N/A | N/A | 3.00% | 3.00% | 6.00% | 2.00% | 3.00% | 2% < 10Mil, 4%>=10Mil | 0.50% | 2.00% | 2% | 3.00% |
| Interest bearing amount | N/A | N/A | 50,000.00 | 50,000.00 | 50,000.00 | 50,000.00 | 50,000.00 | 100,000.00 | 5,000.00 | 20,000.00 | 500,000.00 | 20,000.00 |
| Monthly Mantainance fee | 20,000.00 | 10,000.00 | 2,500.00 | 2,500.00 | Free | Free | Free | Free | 2 | Free | Free | Free |
| Deposit | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free |
| Monthly Statement | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free |
| Adhock statement Per page | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 1 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 |

### OTHER CHARGES

| SERVICES | AMOUNT ( TZS) |
|---|---|
| Certificate of Balance | 30,000.00 |
| Confirmation to the Auditors | 30,000.00 |
| Search for information above 5 years | 15,000.00 |
| Cheque book cost (Per Leaf) | 600.00 |
| Status report | 30,000.00 |
| Stop payment order | 30,000.00 |
| Dishonoured cheque for lack of funds or refer to drawer or effect not cleared | 100,000.00 |
| Dishonoured cheque due to the technical error caused by customer | 60,000.00 |
| Dormant Account Activation | Free |
| Account Closing on Customer Demand | 10,000.00 |
| Counter cheque per leaf [Within the Bank] | 15,000.00 |
| Salary Processing fee [ per Transaction] | 1,000.00 |
| Customer ID | 10,000.00 |
| Pre-Mature breaking of Fixed Deposit on customer request | Minimum of 50% of the accrued interest |
| CCTV Camera footage searching request from Customer | 30,000.00 |
| Uncollected Cheque Book/Destruction | 5,000.00 |
| Visa Card Issuance-Classic | 10,000.00 |
| Visa Card Issuance-Gold | 15,000.00 |
| Replacement Visa Card-Classic | 15,000.00 |
| Replacement Visa Card-Gold | 25,000.00 |
| Umoja Card Mantainance fee | 1000 per month |
| Visa Card- Classic Mantainance fee | 3,000 per QTR |
| Visa Card-Gold Mantainance fee | 5,000 per QTR |
| Uncollected ATM Card | 5,000.00 |
| PIN reset fee | 5,000.00 |
| Withdraw fee local (Umoja ATM) | 1000-99,000=1500 100,000-400,000=1700 |
| Withdraw fee other Bank (Domestic Banks) | 3,500 |
| Withdraw fee other Bank (International) | 11,000 |
| Balance inquiry Umoja ATM | 300 |
| Balance inquiry other Domestic Banks | 950 |
| Balance inquiry other Bank (International) | 2,000 |
| Decline Domestic [Insufficient fund] | 1,000 |
| Decline International [Insufficient Balance] | 1,500 |
| QR transactions | 3% of Transaction Amt |
| POS transactions | 3% of Transaction Amt |
| E-commerce transactions | 3% of Transaction Amt |

Cash Withdraw Over the Counter [TZS/ USD/EURO]

| TRANSACTION AMOUNT | RATES |
|---|---|
| Wekeza/Jiwekezee | 2,000.00 |
| Bellow 10 Mil | 3,000.00 |
| Above 10Mill to 50 Mil | 0.10% |
| Above 50Mil t0 100 Mil | 0.090% |
| Above 100Mil to 300 Mil | 0.089% |
| Above 300 Mil | 0.079% |

Cash Withdraw Over the CounterForeign Currency [USD/EURO]

| TRANSACTION AMOUNT | RATES |
|---|---|
| Below USD/EURO 4,000 | 2 |
| Above USD/EURO 4000 | 0.1% more than USD/EURO 40 |

### AGENCY BANKING CHARGES

| TYPE OF SERVICES | RATES |
|---|---|
| Deposit | Free |
| Balance Inquiry | 500 |
| Min Statement | 700 |
| Transfer of fund within MHB | 2,000 |
| Transfer of funds to other Bank | 13,000 |

### AGENCY BANKING WITHDRAWAL FEE

| AMOUNT | FEE |
|---|---|
| Up to 50,000 | 850.00 |
| 50,000 - 100,000 | 1,000.00 |
| 100,000 - 300,000 | 2,000.00 |
| 300,000 - 500,000 | 3,500.00 |
| 500,000 - 1,000,000 | 4,500.00 |
| 1,000,000 - 3,000,000 | 6,000.00 |
| 3,000,000 - 5,000,000 | 10,000.00 |

### MOBILE BANKING CHARGES

WITHDRAWAL CHARGES

| MINIMUM [TZS] | MAXIMUM [TZS] | RATES [TZS] |
|---|---|---|
| 0 | 10,000 | 800 |
| 10,001 | 19,999 | 1,800 |
| 20,000 | 49,999 | 3,500 |
| 50,000 | 99,999 | 5,200 |
| 100,000 | 199,999 | 7,200 |
| 200,000 | 499,999 | 8,200 |
| 500,000 | 999,999 | 10,500 |
| 1,000,000 | 2,000,000 | 11,200 |
| 2,000,001 | 3,000,000 | 12,000 |
| 3,000,001 | 5,000,000 | 15,000 |

FUND TRANSFER CHARGES

| | |
|---|---|
| Transfer of Funds within MHB | 2,000.00 |
| Transfer of funds to other Banks | 13,000.00 |

### EFT/SWIFT/TISS

| | |
|---|---|
| EFT within the Bank (Incoming) | Free |
| EFT to other Banks | 1,500.00 |
| TISS Transfer | 10,000.00 |
| T.T. Transfer | - |

### STANDING ORDER

| | |
|---|---|
| Instructions within MHB | FREE |
| Standing Order to other Bank | 10,000/= |

www.mhbbank.co.tz

OFISI YA WAZIRI MKUU

KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU

## TAARIFA KWA UMMA

**KUITWA KUANZA MAFUNZO YA UFUNDI STADI ZA KAZI KATIKA FANI MBALIMBALI KWA NJIA YA UANAGENZI**

Tarehe 01 Novemba, 2023 Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu (OWM – KVAU) ilitangaza fursa za mafunzo ambayo yatatolewa katika taasisi za mafunzo zilizotangazwa kutoka Mikoa 26 ya Tanzania Bara. Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu inapenda kuutaarifu umma kuwa vijana 6,000 wamechaguliwa kujiunga na mafunzo katika vyuo 43 nchini. Majina ya vijana waliochaguliwa yamebandikwa kwenye mbao za matangazo za vyuo husika na katika tovuti ya www.kazi.go.tz . Vijana waliochaguliwa wanatakiwa kuripoti kwenye vyuo hivyo kwa ajili ya kuthibitisha na kujisajili kuanzia tarehe 15 Januari, 2024 ambapo mafunzo yataanza rasmi tarehe 22 Januari, 2024. Mikoa na vyuo ambapo mafunzo yatafanyika ni kama ifuatavyo:-

| MKOA | JINA LA CHUO |
|---|---|
| ARUSHA | 1. DON BOSCO KII –TECH |
| | 2. CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI MTO WA MBU |
| DAR ES SALAAM | 3. DSM RVTSC |
| | 4. DON BOSCO OSTERBAY VTC |
| DODOMA | 5. INSTITUTE OF HEAVY EQUIPMENT AND TECHNOLOGY |
| | 6. DON BOSCO DODOMA TECHNICAL INSTITUTE |
| GEITA | 7. GEITA VOCATIONAL TRAINING CENTRE |
| IRINGA | 8. CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI ILULA |
| | 9. MAFINGA LUTHERAN VOCATIONAL TRAINING CENTRE |
| | 10. RDO KILOLO VOCATIONAL TRAINING CENTRE |
| KAGERA | 11. CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI RUBONDO |
| | 12. CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI GERA |
| KATAVI | 13. CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI MSAGINYA |
| KIGOMA | 14. CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI KASULU |
| | 15. CHUO CHA UFUNDI STADI JKT KASANDA |
| | 16. CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI KIHINGA |
| | 17. KASULU DVTC |
| KILIMANJARO | 18. CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI MAMTUKUNA |
| | 19. MARANGU SCHOOL OF TOURISM AND VOCATIONAL TRAINING |
| LINDI | 20. CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI KILWA MASOKO |
| | 21. RUANGWA DVTC |
| MANYARA | 22. CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI TANGO |
| MARA | 23. ST.ANTHONY VOCATIONAL TRAINING CENTRE |
| MBEYA | 24. CHUO CHA UFUNDI MAGEREZA RUANDA |
| MOROGORO | 25. LAKEWOOD TRAINING INSTITUTE |
| MTWARA | 26. CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI MASASI |
| MWANZA | 27. MWANZA RVTSC |
| | 28. CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI SENGEREMA |
| NJOMBE | 29. CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI NJOMBE |
| PWANI | 30. PWANI RVTSC |
| RUVUMA | 31. CHUO CHA UFUNDI STADI MPAPA |
| | 32. PERAMIHO VOCATIONAL TRAINING CENTRE |
| RUKWA | 33.LAELA AGRICULTURE VTC |
| | 34.CHUO CHA SAYANSI NA TEKNOLOJIA MBEYA (MUST RUKWA) |
| SHINYANGA | 35.HILL FOREST COLLEGE - KAHAMA |
| SIMIYU | 36.CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI BARIADI |
| SINGIDA | 37.CHUO CHA UFUNDI NA MAREKEBISHO KWA WATU WENYE ULEMAVU SABASABA |
| | 38.CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI SINGIDA |
| SONGWE | 39. ILEJE DVTC |
| TABORA | 40.CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI MWANHALA |
| | 41.URAMBO DVTC |
| TANGA | 42.ST.PATRICK'S VOCATIONAL TRAINING CENTER |
| | 43. CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI HANDENI |

IMETOLEWA NA:

KATIBU MKUU


# Mtoto asimulia alivyolea wadogo zake 6 bila msaada wa wazazi

**Ibrahim Joseph,** IKUNGI

FAMILIA ya watoto saba wenye umri chini ya miaka 10 imesimulia ilivyojitunza yenyewe kwa miaka mitatu kutokana na wazazi wao kutengana.

Watoto hao wameibuliwa na kampeni ya huduma ya msaada wa kisheria ya Mama Samia inayoendelea wilayani hapa iliyozinduliwa Januari 10, mwaka huu.

Nipashe iliongea na mmoja wa watoto hao walipofika makao makuu ya Wilaya ya Ikungi kukutana na timu ya kampeni hiyo iliyowaita baba, mama na watoto hao ili kupata chanzo ya tatizo.

Akizungumzia tukio hilo, mmoja wa watoto wa familia hiyo (jina linahifadhiwa) alisema wanajitunza kwa muda wote huo kutokana na wazazi wao kutengana na mama yao kwenda kuishi nyumbani kwao.

Watoto hao wanakaa na baba yao, Temistocules Ijengo, ambaye hawahudumii kutokana na kushinda muda mwingi kwenye pombe. Alisema mama yake aliondoka na kuwaacha watoto hao sita huku mmoja akiwa chini ya umri wa miaka miwili ambaye alimtunza mpaka sasa amefika umri wa miaka minne.

Alisimulia kuwa kwa sasa anasoma shule ya msingi, lakini hahudhurii masomo vizuri kutokana na kutumia muda mwingi kuwahudumia wadogo zake kwa kuomba omba chakula kwa watu.

Alisema wakizidiwa na njaa huenda kwa mama yao kuomba msaada wa chakula na kumwekea baba yao chakula kinachopatikana kwa kuwa wanampenda na wasingependa kuona anakufa kwa njaa. Kiongozi wa timu ya kampeni ya huduma ya msaada wa kisheria Wilaya ya Ikungi, Laurent Burilo, akizungumza na waandishi wa habari wilayani humo jana, alisema wakiwa katika Kijiji cha Mwisi wilayani hapo kwa ajili ya kutoa elimu ya msaada wa kisheria, walipata taarifa ya watoto hao kupitia viongozi wa kijiji hicho.

Burilo alisema baada ya taarifa hizo walichukua jukumu la kuwatafuta wazazi hao na walifanikiwa kukutana nao na kufanya mazungumzo na wote wawili.

Kadhalika alisema kuwa walianza kufanya mazungumzo na mmoja mmoja na kuwaeleza madhara ya maisha ya watoto wao na ndipo walipowakutanisha na kufanikiwa kuwaunganisha tena familia hiyo pamoja na watoto wao ambao nao walifika katika eneo hilo.

Mmoja wa majirani wa familia hiyo, Emanuel Ntandu, aliyeshiriki kuwasafirisha watoto hao pamoja na baba yao kutoka kijijini hadi makao makuu ya wilaya, alisema wamekuwa wakiwasaidia chakula watoto hao mara kwa mara na wamekuwa wakilalamikia tatizo hilo kwa muda.

Aliishukuru kampeni hiyo ya mama Samia kwa kufika na kuwasaidia watoto hao ambao wameishi kwa shida muda huo wa miaka mitatu. Mama wa watoto hao, Neema Joseph, akizungumza na waandishi wa habari, alisema aliikimbia ndoa yake kutokana na unyanyasaji kutoka kwa mume wake.

Alisema siku ya mwisho kuondoka alishuhudia mume wake akiwapiga watoto na alipohoji naye alipigwa akaona bora aokoe uhai wake. Ofisa Ustawi Wilaya ya Ikungi, Beatrice Maeda, alisema baada ya kufanikiwa kuiunganisha familia hiyo, wataendelea kuifuatilia na Temistocules atakuwa akiripotia Ofisi ya Mtendaji wa Kijiji kila siku kwa muda wa mwezi moja kuangalia mwenendo wake na taarifa hizo zitakuwa zikifikishwa kituo cha polisi kila siku

Alisema, endapo atakiuka masharti hayo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake kwa sababu ndiye aliyeonekana kusababisha familia hiyo kutengana.

# WMA, ZAWEMA zatia saini mkataba kushirikiana

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Vipimo Tanzania Bara (WMA) na Wakala wa Vipimo Zanzibar (ZAWEMA), umetia saini hati ya makubaliano ya ushirikiano (MoU) ili kuimarisha utendaji kazi wao katika maeneo mbalimbali.

Maeneo watakayoshirikiana ni kubadilishana utaalamu na vitendea kazi ili kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi wanaowahudumia kwa upande wa Bara na Visiwani Zanzibar.

Akizungumza baada ya kushuhudia utiaji saini huo, kituo cha maonesho ya biashara Nyamanzi Fumba, Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara Serikali ya Zanzibar, Dk. Hashil Abdallah, alisema ni vyema kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi hizo ili kuhakikisha vipimo vyote vinakuwa sahihi na mnunuzi wa bidhaa anapata kulingana na thamani ya fedha anayotoa.

Dk. Hashil alisema, kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo, wakala wa vipimo ndiyo taasisi pekee inayopaswa kusimamia matumizi sahihi ya vipimo kwa kuhakikisha kuwa vipimo vinavyotumika katika biashara viko sahihi na kuzingatia matumizi sahihi ili kuepusha madhara ili kulinda walaji.

Aidha, alisema makubaliano hayo yatasaidia kuimarisha utendaji kazi na kuongeza ufanisi utakaosaidia kufikia malengo ya taasisi hizo kwasababu WMA ilianzishwa muda mrefu na ina uzoefu wa kutosha na vifaa vingi vya kisasa.

Alisema kwa ushirikiano huo, WMA itaiwezesha zaidi ZAWEMA kutumia pia vifaa hivyo na wataalamu ili kusimamia matumizi sahihi ya vipimo katika sekta nyingi zaidi.

Katibu Mkuu Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar, Ali Khamis Juma, alisema ushirikiano baina ya taasisi za WMA na ZAWEMA ni wa kudumu na utaisadia kukua zaidi na kuingia katika maeneo mengi ya kiutendaji kama ilivyo upande wa WMA Tanzania Bara.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Stella Kahwa, alisema ushirikiano huo umekuwapo muda ingawa haukuwa rasmi kimaandishi.

Alisema mara nyingi WMA na ZAWEMA hushirikiana kuendesha kaguzi mbalimbali visiwani Zanzibar kwa wauzaji wa vito na madini, mafuta na hata katika sekta ya gesi ili kuhakikisha vipimo vinakuwa sahihi wateja hawaibiwi.

Mkurugenzi wa ZAWEMA, Mohammed Simai Mwalim, alisema vipimo vikisimamiwa kwa usahihi katika bidhaa mbalimbali zinazozalishwa nchini na zinazoingizwa kutoka nje ya nchi itasaidia serikali kukusanya kodi kwa usahihi.

Alitoa wito kwa wananchi na wafanyabiashara wote wa Tanzania Bara na Zanzibar kutumia vipimo sahihi na wakikutana na changamoto yoyote inayohusu vipimo wafike kwenye ofisi za Wakala wa Vipimo kwa ajili ya kupata msaada wa kitaalamu.





# NMB yasaidia waathirika mafuriko Hanang' kulipwa fidia ya mil. 270/-

**Na Mwandishi Wetu,**
HANANG'

BENKI ya NMB imesaidia wajasiriamali wadogo na wakati walioathirika na maporomoko ya tope wilayani Hanang' kulipwa fidia ya hasara walizopata kutokana na janga hilo lililotokea mwanzoni mwa Desemba mwaka jana.

Waathirika hao 18 wanaolipwa Sh. milioni 270 na kampuni ya Reliance Insurance walikuwa na mikopo yenye kinga ya bima ya mshirika huyo wa NMB katika biashara ya huduma za bima zinazotolewa na benki (bancassurance) hiyo.

Kulipwa kwa wakati kwa wateja hao wa NMB ni matokeo ya kushiriki kikamilifu kwa taasisi hiyo katika kuyachakata malipo ya madai yao. Ulipaji wake ulitangazwa rasmi wiki jana katika stendi ya mabasi Katesh wakati wa hafla ya kukabidhi mfano wa hundi wa kiasi cha fidia hiyo.

Wazungumzaji kwenye shughuli hiyo hawakusisitiza tu umuhimu wa kukata bima, bali pia walitoa wito kutolewa elimu kuhusu huduma hiyo hasa kwa wananchi wa kawaida ambao ufahamu wao wa masuala na faida za bima bado ni mdogo.

Akifafanua umuhimu wa bima katika maisha na usalama wa mali, Mkuu wa Idara ya Bima ya NMB, Martine Massawe, alisema nafuu ya hasara waliyopata waathirika hao wa mafuriko ya Hanang ni kwa sababu walikuwa na kinga ya bima katika biashara.

Massawe alisisitiza bima ni huduma inayosaidia kuzikabili hatari za kibiashara ambayo wajasiriamali wanapaswa kuhakikisha wanayo ili kujilinda hasa kifedha.

Alisema bima inawasaidia pia kuzirejesha shughuli zao katika hali ya kawaida baada ya kuathirika na majanga kama maafa ya Hanang.

"Wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo hukabiliwa na changamoto nyingi na matukio yasiyotarajiwa, hivyo kutokuwa na uhakika wa usalama uendelevu wa shughuli zao.

"Kwa mantiki hiyo, bima ni kitu muhimu kwa ajili ya kutoa ahueni kwa waathirika wa athari kama hizo ambazo huhatarisha maisha na mafanikio yao," alibainisha.

Akisisitiza dhamira ya NMB kuchochea ukuaji wa matumizi ya bima nchini, ofisa huyo alisema huduma hiyo haitoi tu usalama wa kifedha, bali pia huwahakikishia wajasiriamali amani katika kutekeleza majukumu yao.

Kwa mujibu wa Massawe, ushiriki wa NMB katika bima unalenga hasa kusaidia ustawi wa biashara za ndani kupitia masuluhisho bunifu na pia kuchangia ukuaji wa sekta hiyo nchini.

Ili kutimiza malengo hayo, aliwaomba wakazi wa Mkoa wa Manyara na Watanzania wote kwa ujumla kuzitumia bima mbalimbali zinazotolewa na kuzidi kubuniwa na benki hiyo.

"Benki yetu inazo bidhaa mbalimbali bora za bima ambazo ni mahususi kwa ajili ya kada mbalimbali za wananchi kimapato ambazo bei zake ni nafuu ikiwamo huduma ambayo malipo yake kwa mwaka ni Sh. 10,000. Uzuri ni kwamba taratibu za upatikanaji wake zimerahisishwa ili kuwavutia watu wengi," Massawe alisema.

Alibainisha kuwa mwaka huu benki hiyo itaendeleza kampeni ya 'Umebima' ili kuzidi kuhamasisha matumizi chanya ya bima itakayokwenda sambamba na utoaji elimu nchi nzima kuhusu umuhimu wa huduma hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Hanang, Janeth Mayanja, alisema elimu hiyo inahitajika sana wilayani humo kutokana na watu wengi kuwa na uelewa mdogo wa huduma za bima na jinsi ya kuzipata.

Alisema utafiti wa awali wa kubainisha ukubwa wa janga lililowapata si tu ulibaini kuathirika kwa mamia ya wajasiriamali, bali pia uligundua wengi hawakuwa na bima wala ufahamu wa faida zake.

"Kimsingi, kiwango cha elimu kuhusu huduma za bima katika wilaya yetu bado kiko chini sana na hakuna mtu aliyewahi kufikiria kuwa wilaya yetu ingekumbwa na janga kama hilo," alisema Janeth.

Mmoja wa wanufaika wa fidia hiyo, Hapiness Mlay, ambaye amelipwa Sh. milioni 28.5, alisisitiza umuhimu wa bima na kuwasihi wafanyabiashara wasiokuwa na bima kuhakikisha wanaipata ili kupunguza athari za kutokuwa na kinga hiyo.

Akibainisha kuwa ulipaji wa fidia kwa wakati ni takwa la kikanuni, Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Dk. Baghayo Saqware, aliagiza kampuni za bima kulipa kipaumbele suala la unafuu wa gharama za huduma zinazozitoa.

"Hivi sasa watoa huduma mbalimbali wa bima wamebuni bidhaa mbalimbali za bima ili kuvutia watumiaji wengi.

"Ninatumia fursa hii kukumbusha wananchi wote kuchangamkia fursa hii kikamilifu ili kupunguza athari za majanga," alisema na kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwa mstari wa mbele kuhamasisha utumiaji huduma hizo na kuzidi kupambania Bima ya Afya kwa Wote.




Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Hosea Kashimba (katikati), akimhudumia mwanachama wa mfuko huo katika banda la PSSSF kwenye Maonesho ya 10 ya Biashara ya Kimataifa ya Zanzibar, viwanja vya Nyamanzi, kisiwani Unguja, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CCM kuwang'oa viongozi wasiosoma mapato, matumizi

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Manyara, kimetangaza 'kiama' kwa wenyeviti wa serikali za vijiji, vitongoji na mitaa, ambao hawakuwa na utaratibu wa kusoma mapato na matumizi kwa wananchi, ikiwataka wajiandae kung'oka.

Juni mwaka huu, muhula wa uongozi wa viongozi wa kisiasa wa kada hiyo itakuwa umefikia ukomo kwa mujibu wa sheria ili kupisha uchaguzi mwingine unaotarajiwa kufanyika baadaye Novemba mwaka huu.

Akitangaza msimamo huo mwishoni mwa wiki, Katibu Mwenezi wa CCM, mkoani hapa, John Nzwalile, alisema kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika, chama hicho kitapitisha chujio kali dhidi ya wagombea waliozembea.

"Tutawaengua kwa kufanya mchujo ili kuwapata wagombea sahihi. Wale ambao hawakufanya mikutano na kuwasomea wananchi mapato na matumizi, hawatapata nafasi ya kupitishwa kugombea. "Tutaangalia weledi wa wagombea na atakayetoa rushwa kura za maoni mwaka huu, tumejipanga kweli kweli kumshughulikia. ...Watu ambao hawakubaliki kwenye jamii tutawakata. Hatutakubali kuwapitisha na mkoa huu tutaongoza kwa kishindo, maana CCM huwa tunafanya hesabu za kujumulisha siyo za kutoa."

Wakati huo huo, Nzwalile, alisema Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM Taifa, Paul Makonda, anatarajiwa kuanza ziara ya kikazi mkoani humo, kati ya Januari 20 hadi 22 mwaka huu.

Makonda akiwa mkoani Manyara, atafanya mazungumzo na wazee wa Mji wa Babati, Kamati ya Siasa ya Mkoa na atafanya mkutano wa hadhara katika Uwanja wa Motel Papa.

# Kaya 1,069 zajiandikisha kuondoka Hifadhi Ngorongoro

**Na Godfrey Mushi,** KARATU

SERIKALI imesema morali ya wafugaji wa jamii ya Kimasai, inayotaka kuondoka kwa hiari katika eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) inaongezeka kwa kasi, baada ya kaya 1,069 kujiandikisha kuhama.

Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa NCAA, Fedes Mdala, ambaye ni meneja wa mradi huo, alisema Januari 12 mwaka huu, kaya 44 zenye watu 296 na mifugo 1,206 ziliagwa na kuondoka kwenda kwenye makazi mapya yaliyoko Mkoa wa Tanga.

Makazi mapya kwa ajili ya wanaohama katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, mkoani Arusha, yamejengwa na serikali katika Kijiji cha Msomera, Kata ya Misima, Wilaya ya Handeni.

Maeneo mengine yaliyotengwa na serikali, ni Kijiji cha Kitwai kilichoko Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara na Kijiji cha Saunyi, Wilaya ya Kilindi, mkoani Tanga.

"Hadi kufikia Januari 12 mwaka huu, jumla ya kaya 1,069 zimejiandikisha kuhama kwa hiyari ndani ya hifadhi, ambapo kati ya kaya hizo, kaya 633 zenye watu 3,526 na mifugo 16, 896 zimeshahama kutoka ndani ya hifadhi," alifafanua Mdala.

Wakati anaziaga kaya hizo, Kamishna wa Uhifadhi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Richard Kiiza, aliwaomba wananchi waliondoka kuwa mabalozi na kuwaelimisha wale ambao bado hawajiandikisha, kuona faida za kuhama.

"Wenzenu waliokwishahamia Msomera na maeneo mengine, wanaendelea kupata maisha bora kutokana na kujengewa na kuboreshewa huduma zote muhimu za kijamii; na walio wengi wameshaanza shughuli za kilimo na wanategemea kupata chakula cha kutosha," alisema Kamishna Kiiza.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi wenzake waliokubali kuhama, Wilfred Makamero, alisema sababu zilizomfanya akubali kuhama kwa hiari ni kuona wanakohamia kuna huduma zote za kijamii.

"Naishukuru serikali kwa kutupatia huduma zote za maendeleo kwa kipindi chote ambako tumeishi hifadhini mpaka sasa tunapoamua kuhama kwa hiari yetu kuelekea Msomera ili tukapate fursa ya kujiendeleza wenyewe tofauti na tulivyokuwa hifadhi kwani shughuli za kimaendeleo kama kulima haziruhusiwi," alisema Makamero.





## Wanafunzi elimu ya juu wachangia damu kituo cha afya

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANAFUNZI wa elimu ya juu mkoani Shinyanga wamechangia damu katika Kituo cha Afya Kambarage kilichopo katika Manispaa ya Shinyanga, pamoja na kufanya usafi wa mazingira.

Mwenyekiti wa seneti ya vyuo vikuu mkoani Shinyanga kupitia Umoja wa Vijana UVCCM, Said Sultan, akizungumza kuhusu tukio hilo alisema wamefanya hivyo ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema waliona ni vyema katika sherehe za maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar wasikae bila ya kufanya jambo lolote, ndipo wakaamua kuchangia damu na kufanya usafi wa mazingira katika kituo hicho cha afya.

Mganga Mfawidhi katika kituo hicho cha afya, Dk. Ernest Magula, alisema uhitaji wa damu salama hospitalini hapo ni mkubwa kutokana na uhitaji uliopo hasa katika kuokoa maisha ya mama na mtoto wakati wa kujifungua.

Alitolea mfano kwamba kipindi cha Oktoba hadi Desemba mwaka jana walikuwa na uhitaji wa damu salama uniti 319 lakini walikusanya 273 kiasi ambacho hakikutosha.

"Kituo hiki cha afya kina uhitaji mkubwa wa damu salama hasa katika kuokoa maisha ya mama mjamzito, takwimu ambazo tunazo ndani ya mwezi mmoja wanajifungua kina mama 450, na mama akihitaji kuwekewa damu ni zaidi ya uniti tatu, hivyo uhitaji wa damu ni mkubwa tunaomba watu wajitokeze kuchangia damu," alisema Dk.Magula.

Katibu wa CCM Wilaya ya Shinyanga Mjini, Ally Majeshi aliwapongeza vijana hao kwa hatua hiyo waliyoifikia akisema imekuwa mfano na kuacha alama kituoni hapo.

## Wizara yawaita wananchi kushiriki kliniki ya ardhi

**Thomas Wandiba,** SAUT

KAMISHNA Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Mwanza, Happiness Mtutwa, amewaomba wananchi mkoani hapa kujitokeza katika kliniki ya ardhi awamu ya pili.

Kliniki hiyo ilianza Januari 11 ikitarajiwa kumalizika Januari 19 katika Manispaa ya Ilemela, ikiwa na lengo la kutatua kero mbalimbali za ardhi pamoja na kupata hati za ardhi.

Mtutwa alisema kliniki hiyo inalenga kuwafikia wananchi wote ndani ya siku hizo tisa kwani wanafahanu uwepo wa watu waliobanwa na majukumu, hivyo kutoa nafasi kwao katika siku hizo za mapumziko.

"Katika kliniki hii tutatoa hati za ardhi kwa wakati na kuwaepusha wananchi na usumbufu wa kufuatilia hati zao kwa muda mrefu, hivyo niwasihi kutumia siku hizo kikamilifu ili kuhakikisha wanamaliza kero na mahitaji yote ya ardhi,"alisema Mtutwa.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wakazi wa Wilaya ya Ilemela akiwamo Charles Theodor, alisema kliniki hiyo imewasaidia kutatua kero zao, kwamba imesogezwa karibu yao na kuwaepusha na mizunguko ya kufuatilia mkoani.



Mkurugenzi Mtendaji wa AngloGold Ashanti, Alberto Calderon, akitembelea mitambo ya uzalishaji dhahabu ya mgodi wa GGML iliyoko mkoani Geita hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# AngloGold Ashanti yajivunia mazingira bora ya uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

KUTOKANA na mazingira mazuri ya uwekezaji yanayoendelea kuboreshwa na serikali, Kampuni AngloGold Ashanti imetangaza kuanzisha shughuli za utafiti wa madini kupitia kampuni mpya ya Greenfields Mineral Exploration Limited, ikiwa na lengo la kuongeza uzalishaji wa dhahabu nchini.

Uzalishaji dhahabu unafanywa na Kampuni dada ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kwa zaidi ya miaka 20 mkoani Geita. Mkurugenzi Mtendaji wa AngloGold Ashanti, Alberto Calderon, akizungumzia uwekezaji huo, anasema hatua hiyo inaendana na matayarisho ya sherehe za kumbukumbu ya miaka 25 ya GGML nchini.

Anaitaja GGML kama mojawapo ya migodi michache ya dhahabu ya daraja la kwanza duniani, hivyo AngloGold Ashanti wanatarajia kuendeleza kampuni hiyo kwa zaidi ya robo karne ijayo na kuifanya kuwa kampuni pekee ya uchimbaji madini.

AngloGold Ashanti, mzalishaji wa nne kwa ukubwa wa dhahabu duniani, ni kampuni yenye mojawapo ya programu za kimataifa za utafutaji dhahabu ambazo mbali na Tanzania, zinatekeleza majukumu hayo ya uvumbuzi pia katika nchi za Australia, Marekani na Colombia. GGML ambayo ilizalisha wakia yake ya kwanza ya dhahabu mnamo Juni 2000, ni moja ya migodi mikubwa zaidi ya dhahabu ya AngloGold Ashanti iliyo katika mabara matatu, huku uzalishaji mwaka huu ukitarajiwa kuwa takriban wakia 500,000.

AngloGold Ashanti imewekeza kwa kiasi kikubwa katika kuendeleza migodi ya chini ya ardhi kwenye mkataba wa GGML katika ukanda wa dhahabu wa Ziwa Victoria nchini.

Maeneo matatu mapya ya uchimbaji chini kwa chini pamoja na uchimbaji mpya mmoja unaotumia mfumo wa wazi, ni moja ya maeneo yaliyochangia pakubwa uzalishaji dhahabu GGML katika kipindi cha miaka minne. Uwekezaji wa mtaji uliofanywa na kampuni hiyo mnamo mwaka 2023, unatarajiwa kuwa ulifikia takriban Dola za Marekani milioni 193.

Miradi hiyo inatajwa itaongeza maisha ya mgodi kwa miaka kadhaa. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, mpango wa utafiti wa kina kwenye maeneo mgodi ya GGML umepata mafanikio kwa kuongeza wakia milioni 4.8 iliyoongezwa kwenye hifadhi ya madini kulinganishwa na wakia milioni 2.7 iliyozalishwa kwa wakati huo.

Mwaka 2023, kampuni hiyo iliwekeza Dola za Marekani milioni 35 katika utafiti katika eneo la mgodi pekee na imejitolea kuwekeza zaidi ya Dola za Marekani milioni 31 kwa mwaka 2024 kama sehemu ya kampeni yake ya kupanua zaidi maisha ya mgodi huo muhimu.

Sambamba na mkakati endelevu wa AngloGold Ashanti wa kupunguza hewa ya ukaa, GGML inatekeleza mradi wa kuunganisha mgodi huo kwenye Gridi ya Taifa ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), mpango ambao si tu kwamba utapunguza nusu ya gharama ya uendeshaji mgodi, bali pia utakuwa na uwezo wa kupunguza utoaji wake wa kaboni kwa 81Kt $CO_2$-e ifikapo mwaka 2030.

Katika sehemu ya mchango wake katika kuleta thamani ya pamoja na jamii mwenyeji kwa ujumla, GGM tangu kuanzishwa kwake imeshirikiana na serikali kufadhili na kutekeleza miradi ya uwekezaji ya kijamii katika sekta za kimkakati kama vile elimu, afya, maji, barabara na mapato kwa kizazi kijacho.

Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Nyankumbu ambayo imekuwa kitovu cha ubora kwa wasichana katika ukanda wa ziwa, sasa inachukua zaidi ya wasichana 1,000 kuanzia shule za msingi hadi sekondari. Mradi wa Majisafi wa Mji wa Geita na Mradi wa Maji wa Mji huo kwa pamoja umesaidia kuinua idadi ya kaya zinazopata majisafi na salama kwa zaidi ya asilimia 65.

Miradi hiyo pamoja na mingine mingi iliyofanywa kutokana na kuwapo kwa GGML, inaonesha dhamira ya AngloGold Ashanti kuinua ustawi wa jamii ya Geita.

# Madereva watakiwa kuzingatia sheria usalama barabarani

**Na Remmy Moka,** SAUT

WAMILIKI na madereva wa magari ya kubeba wanafunzi wametakiwa kufuata kanuni, taratibu na sheria za usalama barabarani ili kulinda usalama wa wanafunzi, raia wawapo barabarani.

Rai hiyo ilitolewa jana na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, SACP Wilbroad Mutafungwa, wakati akizungumza na wamiliki pamoja na madereva kutoka wilaya za Ilemela na Nyamagana.

Alisema katika utoaji wa huduma hiyo ya usafirishaji kwa wanafunzi ni vyema kutambua na kufuata sheria zote za barabarani ili kuwaweka salama watumiaji wa barabara pamoja na wanafunzi.

Katika hatua nyingine Kamanda Mutafungwa alikemea vitendo vya ulawiti vinavyofanywa na baadhi ya madereva wasio waaminifu kwa wanafunzi, akisema hali inayosababisha kuzima ndoto za wanafunzi.

Aidha alisema Jeshi la Polisi litaendelea kufanya ukaguzi wa magari hayo pamoja na kutoa elimu kwa waendesha vyombo hivyo katika wilaya zote ili kuimarisha hali ya usalama barabarani katika wilaya zote za mkoa huo.

Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Mwanza, Sanday Ibrahim, alisema elimu kwa watoa huduma hao pamoja na wadau ni mahususi katika kuongeza ufanisi kwa kutambua changamoto zinazowakabili katika shughuli zao wanapokuwa barabarani.

Alisema lengo la Jeshi la Polisi ni kuhakikisha usalama barabarani unazidi kudumu kwa usalama wa mwanafunzi na raia wanapokuwa barabarani. Baadhi ya wamiliki na madereva walisema kuwa kupitia elimu hiyo imewasaidia kuwaongezea weledi kwa sababu walikuwa hawafahamu. Hivyo walilitaka Jeshi la Polisi kutumia busara katika ukamataji wa madereva watendao makosa ya usalama barabarani.

Nipashe
Spotika



WACHEZAJI SABA BORA MWAKA 2023 UK. 12-13



# WACHEZAJI WA5 WALIOTENGENEZA NAFASI NYINGI EPL MSIMU HUU

SALAH

## ISIKUPITE

MAKIPA 10 bora wa wakati wote, 10. Sepp Maier (mechi 706, clean sheets 217), 9. Edwin Van der Sar (mechi 821, clean sheets 230), 8. Iker Casillas (mechi 881, clean sheets 330), 7. Manuel Neuer (mechi 752, clean sheets 344), 6. Peter Schmeichel (mechi 566, clean sheets 98), 5. Oliver Kahn (mechi 785, clean sheets 248), 4. Gianluigi Buffon (mechi 975, clean sheets 120), 3. Gordon Banks (mechi 322, clean sheets 55), 2. Dino Zoff (mechi 837, clean sheets 231), 1. Lev Yashin (mechi 358, clean sheets 178).



**LONDON,** England

ILI kushinda michezo, timu zinahitaji kufunga mabao na wachezaji wao wanahitaji kutengeneza nafasi. Nafasi nyingi zinazotengenezwa huleta fursa muhimu za kufunga mabao zinazoundwa na mtu binafsi au timu wakati wa mechi.

Kwa maana kali zaidi, huu ni wakati ambapo ubora wa nafasi iliyoundwa ni wa juu sana, na kupendekeza fursa ya wazi ya kufunga mabao.

Iwe ni uzani mzuri kupitia mpira, krosi sahihi au uchezaji wa busara katika safu ya tatu ya ushambuliaji, takwimu hii hutoa maarifa kuhusu uwezo wa mchezaji kuchanganya ubunifu na ubora wa kiufundi. Wachezaji wanaounda nafasi kubwa husaidia kufungua ulinzi thabiti na kuunda matokeo ya michezo mara kwa mara.

Makala haya inawaangalia wachezaji watano ambao wametengeneza nafasi nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu England hadi sasa msimu huu wa 2023-24...

### #5 Anthony Elanga (Nottingham Forest) - nafasi 9

Je, Manchester United wanaweza kuharibu uamuzi wao wa kumuuza Anthony Elanga kwa Nottingham Forest msimu wa majira ya joto? Tukizingatia jinsi washambuliaji wao walivyokuwa wapuuzi muhula huu, kuna uwezekano mkubwa kwamba 'Mashetani Wekundu' watajutia uamuzi wao wa kumtoa winga huyo raia wa Sweden.

Elanga amekuwa mchezaji muhimu sana kwa Forest msimu huu. Kasi yake na uwezo wa kuchukua pasi umeongeza makali kwenye mchezo wa kushambulia. Elanga pia anaonekana kuimarika kila mchezo unaoendelea na kwa haraka anakuwa mtaji wa thamani kwa klabu yake mpya.

Ametengeneza nafasi tisa kubwa kwenye Ligi Kuu msimu huu. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, amefunga mabao manne na kutoa asisti tano katika mechi 19 kwenye Ligi Kuu ya hadi sasa.

### #4 Bruno Fernandes (Manchester United) - nafasi 9

Mojawapo ya sababu kuu nyuma ya mapambano ya Manchester United hadi sasa msimu huu wa Ligi Kuu England ni kushindwa kwao kutengeneza nafasi. Washambuliaji wa United wameshindwa kutumia nafasi kubwa.

Kukiwa na mchezaji kama Bruno Fernandes, inatisha kwamba kikosi cha Erik ten Hag kimefanikiwa kufunga mabao 21 pekee katika michezo 19 hadi sasa. Uwezo wa kufikiri haraka wa kiungo huyo wa Kireno na kupiga pasi kwa nguvu kunawasaidia kutengeneza nafasi mara kwa mara katika safu ya tatu ya ushambuliaji kwao.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, ametengeneza nafasi tisa kubwa kwenye ligi hadi sasa msimu huu na amefunga mabao matatu na kutoa asisti tatu.

### #3 Kieran Trippier (Newcastle United) - nafasi 10

Kieran Trippier huenda alidorora wiki za hivi karibuni lakini anaendelea kuwa kiungo wa kutegemewa zaidi wa Newcastle United. Mwingereza huyo ni mmoja wa mabeki wa pembeni wenye vipaji vya hali ya juu wanaocheza Ligi Kuu England kwa sasa.

Ufanisi wa Trippier umekuwa ishara ya mabadiliko ambayo 'Magpies' hao wamepitia chini ya Eddie Howe kwa miaka kadhaa iliyopita. Uwezo wake wa kutoa krosi kwenye maeneo ya hatari umekuwa sehemu muhimu ya uchezaji wao wa kushambulia.

Uwezo wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 ni wa ajabu pia. Ametengeneza nafasi 10 kubwa kwenye Ligi Kuu hadi sasa msimu huu na ametoa pasi saba za mabao saba pia.

### #2 Trent Alexander-Arnold (Liverpool) - nafasi 12

Uwezo wa kiuchezaji wa Trent Alexander-Arnold ndio msingi wa mikakati ya Jurgen Klopp ya kushambulia ya Liverpool. Mlinzi huyo mchanga wa kulia ana uwezo wa ajabu wa kutoa krosi nzuri ndani ya eneo la hatari na pia kunyunyizia mipira mirefu kwa washambuliaji wake.

Baada ya kustahimili hali ya kutofautiana katika msimu wa 2022-23 ambapo Liverpool ilitatizika, Alexander-Arnold amerejea katika ubora wake msimu huu. Ametengeneza nafasi 12 kubwa kwa 'Wekundu' hao kufikia sasa msimu huu na amefunga mabao mawili na kutengeneza pasi nane za mabao.

### #1 Mohamed Salah (Liverpool) - nafasi 14

Mohamed Salah ataingia kwenye historia kama gwiji wa Ligi Kuu England kutokana na uchezaji wake chini ya winga ya kulia ya Liverpool tangu ajiunge na klabu hiyo mwaka 2017. Amekuwa mchezaji wao muhimu zaidi katika zama za Jurgen Klopp kutokana na uwezo wake wa kufunga mabao na kucheza.

Salah, mara nyingi zaidi, hutafuta njia ya kushawishi kila mchezo anaocheza. Ustadi wake wa kuchezea chenga, kasi, wepesi na uwezo wa kupiga pasi za kusisimua ndani ya safu ya tatu ya ushambuliaji humfanya kuwa mshambuliaji wa kiwango cha kimataifa ambaye mabeki hawapendi kuja dhidi yake.

Salah ametengeneza nafasi 14 kubwa kwenye Ligi Kuu msimu huu. Amefunga mabao 12 na kutoa asisti saba katika mechi 19 alizocheza kwenye Ligi Kuu England hadi sasa msimu huu.

# WACHEZAJI SABA BORA MWAKA 2023

**LONDON,** England

NANI mwanasoka bora wa 2023? Ni swali gumu sana kujibu na karibu haiwezekani kuweka sifuri kwa mtu mmoja kwa sababu ambazo tunapaswa kuzingatia. Kwanza kabisa, uchezaji wa mtu binafsi na ushawishi wa jumla ambao mchezaji amekuwa nao kwenye mafanikio ya timu yake unahitaji kuzingatiwa.

**Uthabiti kwa mwaka mzima bado ni kipengele kingine muhimu kwani ubora endelevu mara nyingi hutofautisha wachezaji wa kipekee. Mafanikio, kwa upande wa bidhaa za fedha na sifa za mtu binafsi, lazima yaangaliwe pia.**

Zaidi ya hayo, mambo kama vile uongozi, maadili ya kazi na uwezo wa kufanya kazi katika hali zenye shinikizo kubwa pia yanahitaji kuzingatiwa pia.

Bila kuchelewa zaidi, acha tuangalie wanasoka saba bora zaidi wa mwaka 2023...

### #7 Cristiano Ronaldo (Ureno/Al-Nassr)

Ajabu ya kutosha, Cristiano Ronaldo aliokoa sura ya mwisho ya ufufuo kwa jioni ya kazi yake. Amekuwa mfungaji mabao muhimu kwa klabu na nchi mwaka 2023, ingawa kwa sasa anacheza katika Klabu ya Saudi Pro League, Al-Nassr.

Mshindi huyo mara tano wa tuzo ya Ballon d'Or amefunga mabao 53 mwaka 2023, mabao mengi zaidi ya mchezaji yeyote duniani. Ni ushuhuda wa moyo wake wa kutosema-kufa na uwezo wake wa ajabu wa kufunga mabao.

### #6 Mohamed Salah (Misri/Liverpool)

Mohamed Salah yuko njiani kupata hadhi ya hadithi kwenye Ligi Kuu ikiwa bado hajaipata. Mfalme wa Misri amekuwa mchezaji muhimu zaidi wa Liverpool tangu alipotua klabuni hapo msimu wa majira ya joto wa 2017.

Salah anachanganya kasi, ustadi wa kiufundi, ujasiri na maono ya kuipeleka Liverpool juu karibu kila mara anapoingia kwenye uwanja wa mpira. Uthabiti wake umekuwa wa kustaajabisha na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, amekuwa katika kiwango bora kwa 'Wekundu' hao msimu wa 2023-24.

Kuanzia msimu wa 2022-23, ambao alifunga mabao 30 na kutoa asisti 16 katika mashindano yote, Salah tayari ameshapachika wavuni mabao 16 na kutoa pasi nane za mabao hadi sasa.

### #5 Harry Kane (England/Bayern Munich)

Harry Kane alitumia kipindi cha kwanza cha 2023 katika kikosi cha Tottenham Hotspur, lakini alikuwa akifunga mabao mara kwa mara.

Kane alifunga mabao 30 ya Ligi Kuu England msimu wa 2022-23 kabla ya kumaliza msururu wake wa kutotwaa taji Kaskazini mwa London na kabla ya uhamisho wa pauni milioni 100 kwenda Bayern Munich.

Utajiri wake umeimarika sana huko Bavaria na Kane amekuwa mshambuliaji wa kati aliye katika kiwango bora zaidi kwenye ligi tano bora za Ulaya katika kampeni ya 2023-24.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, amefunga mabao 25 na kutoa asisti nane katika mechi 22 kwenye michuano yote akiwa na Bayern Munich hadi sasa msimu huu.



KYLIAN MBAPPE

### #4 Rodri (Hispania/Manchester City)

Rodri ndiye moyo na roho ya Manchester City. Yeye ni mtu muhimu sana, kwamba bila yeye kutamba katikati ya uwanja, City mara nyingi huvunjika kwa kishindo. Anacheza vizuri sana kutoka kwa kina huku pia akionesha uwezo wa ajabu wa 'kuvunja' washambuliaji wa upinzani kwa kuchanganya uchezaji wake wa riadha na mbinu.

Rodri pia anachangia upande mwingine wa uwanja na mabao muhimu. Alikuwa mmoja wa wachezaji thabiti na wa kutegemewa wa City waliposhinda mataji matatu msimu uliopita. Rodri pia alishinda Ligi ya Mataifa ya UEFA akiwa na Hispania katika msimu wa majira ya joto na 2023 umekuwa mwaka wa kutosahaulika katika taaluma yake.

### #3 Jude Bellingham (England/Real Madrid)

Jude Bellingham tayari amepata kiti chake kule Real Madrid. Kwa uchezaji wake wa kuigwa katika safu ya kiungo, nusura aongoze Borussia Dortmund kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, msimu uliopita.

Ingawa yote hayo yalikuwa mazuri kwa mtu mdogo sana, bado hatukujitayarisha kwa yale tuliyokuwa karibu kushuhudia katika kipindi chake cha kwanza cha nusu msimu katika klabu kubwa kama Real Madrid. Bellingham amekuwa muhimu sana katika kikosi cha Real Madrid kwa msimu wa 2023-24.

Katika mechi 21 kwenye michuano yote kwa kikosi cha kocha, Carlo Ancelotti hadi sasa msimu huu, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, amefunga mabao 17 na kutoa asisti tano.

### #2 Erling Haaland (Norway/Manchester City)

Erling Haaland alizitia hofu timu za Ligi Kuu England kwa uwezo wake wa ajabu wa kufunga mabao katika msimu wa 2022-23. Alivunja rekodi nyingi ikiwa ni pamoja na mabao mengi zaidi katika kampeni moja ya Ligi Kuu (36). Mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway alichangia kwa kiasi kikubwa ushindi wa mataji matatu ya Manchester City msimu uliopita.

Haaland anachukuliwa kuwa mshambuliaji bora wa kati katika mchezo huo hivi sasa na bado ana umri wa miaka 23 tu. Amekuwa katika kiwango kizuri msimu wa 2023-24 pia na hadi sasa amefunga mabao 19 na kutoa pasi tano za mabao kwenye mechi 22 katika mashindano yote Man City.


### #1 Kylian Mbappe (Ufaransa/Paris Saint-Germain)

Kylian Mbappe anaendelea kuwanyanyasa wapinzani katika soka la daraja la juu. Alikuwa katikati ya sakata la uhamisho majira ya joto, lakini Mfaransa huyo alirejea uwanjani kuwakumbusha Paris Saint-Germain jinsi alivyo maalum.

Mbappe ni aina ya mwanasoka anayeweza kuifanya dunia nzima kusimama na kuchukua tahadhari. Alikuwa mfungaji bora katika msimu wa 2022-23 wa Ligue 1 na tayari yuko njiani kufikia mafanikio hayo msimu huu. Amefunga mabao 21 na kutoa pasi mbili za mabao katika mechi 22 alizocheza kwenye mashindano yote akiwa na PSG hadi sasa msimu huu. Mbappe ni mshambuliaji asiyeweza kushindwa.

## Nukuu

"Ikiwa unataka kuonyesha ubora, unahitaji wachezaji wenye njaa. Tunahitaji watu wenye haiba na wachezaji ambao wana njaa sana kupigania beji na klabu hii," **Kocha wa Manchester United, Erik ten Hag.**



"Nadhani Olivier Giroud [ndiye mshambuliaji mkali zaidi ambaye nimecheza dhidi yake]. Kila wakati, unafikiri umemshikilia, lakini huwa anafanikiwa kufunga kwa njia moja ama nyingine: kwa kichwa chake, mguu wake, goti lake. Mara nyingi amenifunga (anatabasamu)," **Beki wa kati wa Liverpool, Virgil van Dijk, akimtaja mchezaji wa zamani wa Chelsea na Arsenal, Giroud kuwa ndiye mshambuliaji mgumu zaidi aliyewahi kucheza dhidi yake.**



"[Lionel] Messi anastahili heshima zote na kwa kweli hapa Ufaransa, hakupokea heshima anayostahili," **Nyota wa PSG, Kylian Mbappe.**



Na Adam Fungamwango

# USAJILI DIRISHA DOGO UTAKAOTIKISA LIGI KUU



SARR

DIRISHA la uhamisho kwa klabu za Ligi Kuu Tanzania Bara linatarajiwa kufungwa leo Jumatatu saa 5 na dakika 59 usiku.

**Tangu Desemba 16, mwaka jana lilipofunguliwa, viongozi wa klabu walikuwa wakihaha huku na kule kusaka wachezaji ndani na nje ya nchi ili kutimiza matakwa na mapendekezo ya mabenchi yao ya ufundi.**

Mpaka wakati huu kuna usajili wa wachezaji ambao umekamilika, na zingine bado zipo kwenye tetesi, ambapo kuanzia kesho mbivu na mbichi zitajulikana.

Kila klabu itaweka wazi ni nani iliyomsajili na nani iliyomuacha ingawa wenyewe tayari wanajua hilo. Kuna sajili zilizokamilika ambazo tayari zimeshashtua mashabiki wa soka nchini, ambao wanatarajiwa kuwa wachezaji waliosajili watafanya vizuri kwenye klabu walizohamia.

Ingawa kufanya vema kwa mchezaji kwenye klabu mpya ni suala kama la kamari hivi, lakini zinaonekana ni bora kipindi hiki cha usajili kutokana na rekodi zao huko walikotoka.

Katika makala haya tumekusanya majina ya wachezaji ambao tayari wameshasajiliwa rasmi na wanaotarajiwa kufanya vema kwenye Ligi Kuu...

**1. Augustine Okra - Yanga**

Amerejea tena nchi Tanzania ambapo alicheza Ligi Kuu msimu wa 2022/23 akiwa na Klabu ya Simba. Wekundu wa Msimbazi walimtema winga huyo, Juni mwanzoni mwaka jana kwa sababu mbalimbali, ikiwamo utovu wa nidhamu na majeraha ya muda mrefu.

Safari hii amejiunga na Yanga akitokea klabu yake ambayo pia alikuwa nayo kabla ya kujiunga na Simba, Bechem United FC.

Kabla ya kujiunga na Simba alikuwa kwenye kiwango bora na hata alipojiunga na timu hiyo alifanya makubwa ingawa kwa muda mfupi.

Aliporejea tena kwenye klabu yake ya zamani, raia huyo wa Ghana, alikiwasha kweli kweli kiasi cha Yanga kuamua kumrejesha tena nchini.

Amecheza mechi moja akiwa na timu yake mpya mjini Zanzibar kwenye Kombe la Mapinduzi dhidi ya KVZ kwa dakika kadhaa tu kabla ya kuumia. Ni mchezaji anayetazamiwa kufanya makubwa katika Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea.

**2. Babakar Sarr - Simba**

Katika kile kinachoonekana kutibu tatizo la kiungo mkabaji asilia, Klabu ya Simba imemsajili raia wa Senegal, Babakar Sarr kutoka Klabu ya US Monastir ya Tunisia.

Katika mechi zake mbili alizocheza robo fainali ya Kombe la Mapinduzi dhidi ya Jamhuri akiingia kipindi cha pili, na nusu fainali dhidi ya Singida Fountain Gate akiwa ameingia kipindi cha pili hakuwa kwenye kiwango kibaya, wala kizuri ambacho wengi walitarajia.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Imani Kajula, alisema mchezaji huyo bado ana uchovu wa safari, pamoja na kutozoeana na wenzake, lakini wanaamini kuwa atakiwasha.

Sarr ndiyo huyu huyu ambaye ametoka kwenye moja kati ya klabu bora Afrika kwa sasa, US Monastir na alicheza dakika 90 akiwa na timu hiyo katika mechi ya Klabu Bingwa ya Nchi za Kiarabu Julai 31, mwaka jana, dhidi ya Al Nassr iliyokuwa na Cristiano Ronaldo.

Mchezaji mwenye wasifu huo ni lazima mashabiki watarajie makubwa kutoka kwake.

**3. Mohamed Mustafa - Azam FC**

Uzuri ni kwamba msimu huu huu, mashabiki wa soka Tanzania walimuona akikaa langoni katika mechi zote mbili ambazo timu yake ya zamani, El Merrikh ya Sudan ilicheza dhidi ya Yanga.

Ilikuwa ni mechi za raundi ya kwanza, Ligi ya Mabingwa Afrika, ambapo pamoja na kushindwa kuizua Yanga kutinga makundi, ikishinda mabao 2-0 nchini Rwanda na bao 1-0 nchini, lakini alikuwa kikwazo kikubwa kwa timu hiyo kupata ushindi mnono.

Azam imemsajili kipa huyo kwa mkopo wa miezi sita, lakini kwa uwezo ule aliouonesha anatarajia kufanya vema kwenye Ligi Kuu na huenda asiondoke nchini baada ya msimu kumalizika.

**4. Shekhan Ibrahim Khamis - Yanga**

Ni kinda aliyesajiliwa na Yanga kutoka Klabu ya JKU ya Zanzibar. Kwa muda mfupi tu ambao ameichezea timu hiyo ameonekana atakuwa msaada mkubwa kwa kikosi hicho kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na hazina kwa baadaye.

Mchezaji huyo anayecheza nafasi ya winga na kiungo mshambuliaji, anaonekana kuwa na kitu cha ziada nacho ni kupiga mashuti makali ya mbali kama ambavyo alikuwa akifanya, Feisal Salum 'Fei Toto' enzi hizo akiwa na timu hiyo.

**5. Saleh Karabaka - Simba**

Alitumia dakika chache tu kufunga bao, alipoingia kwenye mechi kati ya timu yake mpya, Simba dhidi ya timu yake ya zamani, JKU.

Amecheza baadhi ya mechi kadhaa baada ya hapo na kuonekana ana kipaji, pia haogopi wala kuwa na wasiwasi anapokuwa na mpira akiwa na timu kubwa ya Simba. Hata mechi ya fainali aliyocheza juzi.

Anatarajiwa kuwa mchezaji ambaye mpaka mwisho wa msimu anaweza kufanya makubwa.

**6. Reliants Lusajo - Mashujaa FC**

Ni mmoja kati ya mastraika wachache wa Kitanzania ambao angalau akifika langoni unaweza ukawa na matumaini ya kupata bao. Amekuwa ni mmoja wa wachezaji wanaowania Kiatu cha Dhahabu Ligi Kuu karibuni kila msimu, ingawa hadi leo hajafanikiwa kukitwaa.

Amejiunga na Mashujaa FC akitokea Namungo, ambapo amewahi pia kuichezea KMC na kote huko amekuwa ni moto wa kuotea mbali. Ni moja kati ya wachezaji wanaotarajiwa kutikisa Ligi Kuu akiwa na timu yake hiyo mpya.

**7. Franklin Navarro - Azam**

Mashabiki wengi wa soka walimuona katika mechi ya Kombe la Mapinduzi dhidi ya Chipukizi, walikubali na kusema, "huyu ni mchezaji, na ana kitu."


Huyo ni Franklin Navarro raia wa Colombia aliyesajiliwa na Azam FC. Kwa uchezaji wake akionekana kuwa ni mwepesi na ana maamuzi ya kupiga mashuti ya mbali, anaweza kuwatetemesha makipa wengi nchini ambao wana tabia ya kujisahau kwa sababu mastraika wengi kwa sasa hawana tabia ya kupiga mashuti nje ya eneo la hatari.

**8. Ladack Chasambi - Simba**

Ni mchezaji asiyehitaji maelezo mengi, kwani wengi wanamfahamu tangu akiichezea timu ya vijana ya Mtibwa Sugar chini ya miaka 20. Ameonekana akiichezea Simba kwa mara ya kwanza katika mechi ya fainali dhidi ya Mlandege.

Angalau kuingia kwake yeye na Karabaka kuliifanya timu kuchangamka, licha ya kufungwa bao 1-0. Ni moja kati ya usajili bora na kwa kiasi kikubwa anaweza kuwa mmoja wa wachezaji tegemeo kwa Simba si katika mechi za Ligi ya Mabingwa na Ligi Kuu tu, bali kwa kikosi hicho siku za baadaye.

**JE, WAJUA?**



HAWA ndio manahodha watano bora wa timu za taifa kwa sasa, #5 Luka Modric (Croatia), #4 Harry Kane (England), #3 Kylian Mbappe (Ufaransa), #2 Cristiano Ronaldo (Ureno), #1 Lionel Messi (Argentina).



# Mkalama watakiwa kutogomea shughuli za maendeleo

Na Thobias Mwanakatwe, MKALAMA

WIZARA ya Katiba na Sheria, imewataka wananchi wa Wilaya ya Mkalama mkoani Singida kutogomea shughuli za maendeleo kwa sababu ya migogoro inayojitokeza kwenye vijiji vyao.

Badala yake wametakiwa wajenge utamadauni wa kuzipeleka kero zinazowasibu katika mamlaka husika ili ziweze kupatiwe ufumbuzi.

Wakili kutoka wizara hiyo, Anton Elias, alitoa ushauri huo juzi wakati akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Ilongo Kata ya Ibaga, kwenye mkutano wa hadhara katika kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia inayoendelea wilayani hapa.

Alitoa kauli hiyo baada ya wananchi hao kumlalamikia mmoja wa wananchi wa wilaya hiyo, Mayunga Ng'wigulu kuvamia eneo la malisho lililotengwa na serikali ya Kijiji cha Ilongo.

"Niwaombe ndugu zangu wa Ilongo kugomea shughuli za maendeleo hakuleti suluhu ya mgogoro wenu, kinachotakiwa kukijitokeza migogoro ipelekeni kwenye mamlaka husika ipatiwe ufumbuzi," alisema.

Alisema kuwa lengo la kampeni hiyo ni kuhakikisha wananchi wanakua na elimu ya masuala ya sheria, aliwataka wananchi hao kutumia kampeni hiyo vizuri kuibua matatizo yanayowasibu katika maeneo yao.

Aidha, aliwataka wananchi kuendelea kuwapa ushirikiano viongozi na kushiriki katika shughuli za maendeleo ili kuendeleza maendeleo ya kijiji chao.

Nao baadhi ya wananchi waliomba serikali kupitia kampeni hiyo kutatua mgogoro huo uliodumu kwa muda mrefu, ambapo walisema takribani hekari 18 zilizovamiwa na mwananchi huyo zinarudi mikononi mwa serikali ya Kijiji.



Mkurugenzi wa Kampuni ya Oryx Gas Tanzania, Araman Benoite (wa pili kulia), Mbunge wa Dodoma Mjini na Waziri wa Madini, Athony Mavunde (wa tatu kulia), Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, Alhaj Jabiri Shekimweri (wa pili kushoto), wakimkabidhi mtungi wa gesi ya Oryx mamalishe Elizabeth Chiute (kushoto) katika Viwanja vya Nyerere Square mwishoni mwa wiki. Kulia ni Naibu Meya wa Halmashauri ya Wilaya ya Dodoma Mjini, Asma Karama. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mamalishe, babalishe wapewa mitungi, majiko ya kupikia

Na Mwandishi Wetu, DODOMA

MAMALISHE na babalishe zaidi ya 500 kutoka kata 41 mkoani hapa wamepatiwa msaada wa mitungi ya gesi ya Oryx pamoja na majiko, lengo ni kuachana na matumizi ya mkaa na kutumia nishati safi.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutoa msaada huo, Mkurugenzi wa Kampuni ya Oryx, Araman Benoit, alisema mitungi na majiko hayo yanakwenda kurahisisha shughuli zao za kupika.

Benoite alisema mitungi 500 ya gesi ya Oryx na majiko waliyotoa ina thamani ya Sh.milioni 41 na kwamba wataendelea kufuata maelekezo ya serikali inayohamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Alisema wanaamini kupika kwa gesi kunalinda mazingira kwa kuacha kukata kuni na mkaa lakini inalinda afya kwa kuwaepusha kuvuta moshi na mvuke unaoathiri mapafu na afya zao.

Alisema kwa kutumia nishati safi ya kupikia inayotokana na gesi wanawake wanatumia muda mchache kupika, hivyo wanapata nafasi kufanya shughuli nyingine za maendeleo.

Mbunge wa Dodoma Mjini, Athony Mavunde, aliishukuru kampuni hiyo kwa kutoa msaada huo akisema wamejipanga vizuri katika kuhakikisha wanaenzi kampeni ya kutunza mazingira.

Alisema anaishukuru Kampuni ya Oryx kwa kukubali ombi lao la kuwashika mkono baba na mamalishe wa Dodoma Mjini kwa kuwapatia msaada huo.

"Nichukue fursa hii kumshukuru Rais Samia Samia Suluhu Hassan ambaye yeye ndiye mwasisi wa utunzaji mazingira kwa kutumia nishati safi na alitoa maelekezo kwamba ifikapo mwaka 2032 basi asilimia 80 ya wananchi wawe wanatumia nishati safi ili kuondokana na uchafuzi wa mazingira ambao umesababisha mabadiliko ya tabianchi kwa kiwango kiwango kikubwa," alisema.

Alisema kampeni ya Rais Samia kuhamasisha nishati safi inakwenda kuokoa maisha ya baba na mama lishe ambao kwa sehemu kubwa muda wao mwingi unatumika kupika na wengi wao wanatumia kuni na mkaa.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, Alhaj Jabiri Shekimweri, alimpongeza Mavunde kwa namna anavyojitoa kwa ajili ya wananchi wa Dodoma Mjini wakiwamo baba na mama lishe. Meneja Masoko wa Oryx Gas, Peter Ndomba alitoa mafunzo ya matumizi salama ya nishati safi ya kupikia ya gesi, lengo likiwa ni kuchukua tahadhari ya kuepuka madhara yanayoweza kutokea kwa kutozingatia usalama wakati wa kutumia jiko la gesi.

# Wajitokeza kutoa maoni kufutwa Ofisi Msajili wa Hazina

Na Paul Mabeja, DODOMA

WADAU mbalimbali wamejitokeza kutoa maoni kuhusu Muswada wa Uwekezaji Mitaji ya Umma ambao unalenga kuanzishwa kwa Mamlaka ya Uwekezaji Tanzania itakayofuta Ofisi ya Msajili wa Hazina.

Lengo la kuudwa kwa mamlaka hiyo linatajwa kuwa ni kuongeza ufanisi kwenye utendaji wa mashirika ya umma ambayo hivi sasa yanaonekana kukosa tija licha uwekezaji mkubwa unaofanywa na serikali.

Mmoja wa wadau waliofika kutoka maoni ni wakili na msuluhishi Stephen Msechu ambaye alisema sheria hiyo ni nzuri na imekuja kwa wakati muafaka na italeta tija kwa mashirika ya umma.

Alitaja vifungu ambavyo vitaongeza ufanisi katika utendaji kazi wa mashirika kuwa ni pamoja na Kifungu cha 15 ambacho kinatoa utaratibu shirikishi wa kuhamasisha mali za shirika la umma.

"Kifungu cha 16 kinahakikisha mashirika ya umma yanaongozwa na watu wenye uwezo. Kifungu kingine kinaeleza kuwa kiongozi mmoja haruhusiwi kuongoza taasisi zaidi ya moja hii inaongeza ufanisi na kugawa fursa kwa wengine," alisema.

Naye mwanahabari Absolumu Kibanda, alisema ni muswada ambao msingi wake umejengwa kwa uzoefu wa mafanikio katika nchi zilizo na mfumo uliopendekezwa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji Mitaji ya Umma (PIC), Deus Sangu, akizungumza na waandishi wa habari baada ya wadau kutoa maoni alisema lengo la muswada huo ni kufanya marekebisho kwenye Ofisi ya Msajili wa Hazina ambayo ilikuwa na majukumu ya kusimamia mashirika ya umma.

"Tangu kuanzishwa kwa ofisi ya msajili wa hazina kumekuwa na ombwe kwenye uendeshaji wa mashirika ya umma. Endapo Bunge litaridhia kupitisha muswada huo tutafuta Ofisi ya Msajili wa Hazina na kuanzisha Mamlaka ya Uwekezaji Tanzania ambayo itakuwa na dhima ya kusimamia kwa ukaribu mashirika ya umma," alisema.

Sangu alisema kwa mujibu wa takwimu hadi kufikia Juni mwaka jana kulikuwa na mashirika ya umma 304.

Alisema serikali imewekeza zaidi ya Sh.trilioni 76.7 katika mashirika hayo ambapo fedha hizo ni bajeti ya miaka miwili ya nchi.

Alisema baada ya muswada huo kupitishwa utaanzishwa Mfuko wa Uwekezaji ambapo utahakikisha mashirika yote yanakuwa na mitaji ya kutosha kwa ajili ya kujiendesha.

"Tumepokea maoni ya wadau zaidi ya 50 na tunaendelea kupokea kupitia ofisi ya Bunge baada ya hapo kamati itakaa kwa ajili ya kuyachakata na kuwasilisha ndani ya Bunge ili kuridhia kuwa sheria kamili ambayo itaanzisha taasisi mpya.

"Tunaamini sheria hii ikipita kutakuwa na mambo mazuri ikiwamo wakurugenzi wa bodi za taasisi kuteuliwa kwa njia ya ushindani ambapo wale wenye sifa ndio watapata nafasi," alisema.



# Mvua yabomoa makaburi, yasomba miili iliyozikwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MVUA inayoendelea kunyesha mkoani hapa imeleta athari kwa wananchi wa Kata ya Iganzo baada ya kubomoa makaburi na kusomba miili iliyozikwa.

Tukio hilo lilitokea juzi ambapo baadhi ya wananchi hao walilazimika kuanza kuhamisha miili ya ndugu zao na kwenda kuzika sehemu nyingine ambayo ni salama.

Wakizungumza na waandishi wa habari wakati wa kuhamisha baadhi ya makaburi, wananchi hao walisema chanzo cha mafuriko hayo ni kukosekana kwa mtaro imara kwenye eneo hilo hali ambayo inasababisha maji kuanza kujitafutia njia makaburini.

Mmoja wa wananchi hao, Said Hasham, ambaye ni miongoni mwa waathirika wa kusombewa makaburi yao alisema walimzika mama yao mwaka 2012 jirani na mtaro na hakujawahi kutokea tatizo lolote kwa zaidi ya miaka 10.

Alisema wakati huo mtaro ulikuwa mdogo na hata maji yaliyokuwa yanapita yalikuwa kidogo na kwamba kwa sasa mtaro umepanuka kiasi kwamba umeanza kuathiri makaburi hayo.

“Kwa sasa maji ni mengi na yanazidi kupanua mfereji kiasi kwamba kwa sasa hata kuvuka hatuwezi kuvuka, leo tumekuta kaburi la mama yetu limechimbika kiasi kwamba sanduku linaonekana kwa hiyo tumeamua kuhamisha ili tukazike sehemu nyingine,” alisema Hasham.

Alisema endapo mtaro huo hautadhibitiwa kuna hatari ukaendelea kuathiri makaburi hayo na pengine kuharibu hata makazi ya watu kwa kubomoa nyumba.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Nkuyu yalipo makaburi hayo, Jastin Mwamba alisema awali walimwomba diwani wa kata hiyo, Daniel Mwanjoka awasaidie kufikisha kilio chao halmashauri ili mtaro huo ujengwe kuzuia uharibifu.

Alisema baadaye diwani huyo aliwahakikishia kuwa halmashauri itawasaidia kwa kuujenga mtaro huo jambo ambalo halijatekelezwa mpaka sasa ambapo umeanza kusababisha madhara.

Aliiomba serikali kuwasaidia kwa kuujenga vizuri mtaro huo ili usiendelee kuchimba eneo la makaburi na maeneo ya nyumba za wananchi zilizopo jirani na eneo hilo.

“Tunaomba serikali itusaidie kwa dharura maana kuna makaburi mengine ambayo hayajafikiwa na ndugu hatuwajui, huenda kesho na keshokutwa yakafikiwa na kufukuliwa, sasa hii itakuwa shida zaidi kwetu,” alisema Mwamba.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Iganzo, Bupe Elly alisema baada ya kukuta makaburi hayo yamefukuliwa waliamua kushirikiana na wenye ndugu kuhamisha ili miili isisombwe.



Masta Shangwe (mwenye kofia ngumu), akifurahia na mmoja wa kinamama walionufaika na bima ya bure ya afya kutoka Vodacom Tanzania, Grace John, katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa mwishoni mwa wiki. Kupitia kampeni yake iliyofikia kikomo ya ‘Sambaza Shangwe, Gusa Maisha’, kampuni hii imekabidhi kadi za bima kwa kinamama 100 na watoto 100 hospitalini hapo ikiwa ni zawadi ya upendo katika msimu wa sikukuu uliomalizika.. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DIT yapongezwa kuwatambua, kuwaendeleza wabunifu

**Na Nebart Msokwa,** MOMBA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, ameipongeza Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) kupitia kampuni tanzu ya taasisi hiyo kwa kufanikiwa kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu nchini.

Pongezi hizo zilitolewa jana na Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, wakati akisoma hotuba ya Waziri Mkenda kwenye mahafali ya 17 ya (DIT) Kampasi ya Myunga iliyopo wilayani Momba katika Mkoa wa Songwe.

Alisema kazi inayofanywa na kampuni tanzu ya DIT ya kuimarisha sayansi, teknolojia na ubunifu imekuwa na mchango mkubwa kwa taifa kutokana na kuchangia maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii.

“Ninazo taarifa za kampasi hii kumtumia mmoja wa wabunifu mahiri hapa mkoani Songwe, Adam Kinyekile mwenye karakana yake pale Mpemba Tunduma ambaye serikali ilimfadhili zaidi ya Sh. milioni 99 kwa ajili ya kuendeleza ubunifu wake,” alisema Waziri Mkenda.

Naye mbunifu Adam Kinyekile, alisema DIT kupitia kampuni yake imemsaidia kwa kiasi kikubwa kutambulika ndani na nje ya nchi ambako anauza bidhaa nyingi za kutatua changamoto za kilimo ambazo anazibuni yeye mwenyewe. Aidha, wanafunzi wanaonufaika kwa kiasi kikubwa na kampuni tanzu ya DIT wameonyesha bunifu mbalimbali walizobuni ambazo zinalenga kutatua changamoto mbalimbali katika taifa za uagizaji vifaa kutoka nje ya nchi. Vick Mausa ambaye ni mwanafunzi wa DIT, Dar es Salaam ambaye amefanikiwa kubuni mashine yenye gharama nafuu ya kusaidia wagonjwa wenye matatizo ya figo ambayo itauzwa shilingi milioni nne tofauti na mashine zinazoagizwa nje ya nchi ambazo huuzwa kwa kiasi kikubwa zaidi ya Sh.milioni 20.

Naye Joshua Macha ambaye ni mwanafunzi wa DIT anayesoma mwaka wa kwanza fani ya uhandisi ujenzi alionyesha mashine ya kutengeneza vifaa mbalimbali vya plastiki.

## RC ahimiza wananchi kuchangamkia kilimo cha pareto

**Na Elizabeth John,** MAKETE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, ametoa rai kwa wananchi wa Wilaya ya Makete mkoani hapa kuchangamkia fursa ya kilimo cha pareto ili kiweze kujikwamua kiuchumi.

Alitoa wito huo katika mkutano wa wadau wa pareto na mdau mkuu wa Kampuni ya Pareto Tanzania (PCT) uliofanyika wilayani hapa na kuwajumuisha wakulima wadogo wanaojishughulisha na kilimo hicho ambao ni wanufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Mtaka alisema katika Wilaya ya Makete yenye kata 23, jumla ya kata 21 zenye ukubwa wa hekta 2,800 zinafaa kwa kilimo cha pareto.

“Mimi nataka wakulima watajirike, Makete inawanufaika wa TASAF wapatao 4,569 kwa mwaka wanapata Sh. 144,000 mimi moyoni mwangu hii haikubaliki, tuunganishe kati ya kaya na kaya katika uzalishaji wa pareto ili muondokane na umasikini,” alisema Mtaka.

Mwakilishi wa Kampuni ya PCT kutoka Halmashauri ya Mji wa Mafinga mkoani Iringa, Gerald Joseph, alisema kuwa malengo yao ni kufikia tani 990 kwa sababu hapo awali uzalishaji wa pareto ulikuwa unasuasua.

“Mkulima mwenye hekari moja tukichukuwa wastani wa uzalishaji kwa kilo 250 za maua makavu na ukizidisha kwa Sh. 3, 500 kwa hekari akifuata zile kanuni na taratibu bora za kilimo atapata kwa mwaka mmoja kipato cha Sh. 8,75,000,” alisema Joseph.

Mkuu wa Wilaya ya Makete, Juma Sweda alisema pareto katika wilaya hiyo lilianza mwaka 1931 na kuzalishwa ambapo miaka ya 1990 lilianza kuyumba na kudorora.

Nao baadhi ya wakulima akiwemo, Adrian Sanga alisema pamoja na kuhimiza kufufua zao hilo ni vema pia serikali ikaweka mpango wa kujenga kiwanda wilayani humo.

Wakati huohuo Kampuni ya Pareto (PCT) iligawa miche kwa kaya zaidi ya 267 za wanufaika wa TASAF na kufanya zao hilo kuwa ajenda ya Mkoa wa Njombe.



# ZIC yaja na mpango wa mabadiliko kuchochea utoaji huduma kwa wateja

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Bima la Zanzibar (ZIC) limezindua mpango wake mpya wa kubadili mwonekano na taswira yake kijamii na kibiashara, likilenga kuakisi ukuaji wake sambamba na maboresho ya huduma zake kwa wateja.

Hatua hiyo ya kimkakati inahusisha mfululizo wa mabadiliko chanya yanayohusisha mwonekano mpya wa nembo ya shirika hilo, mwonekano wa nyaraka rasmi za ofisi, maboresho ya huduma kwa wateja na ofisi za shirika hilo.

Hafla ya uzinduzi rasmi wa mwonekano mpya wa ZIC ilifanyika jana Zanzibar, ikiongozwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum, Naibu Kamishna wa Bima Tanzania, Khadija Issa Said, Balozi wa Bima nchini, Wanu Hafidh Ameir, Mwenyekiti wa Bodi ya ZIC, Ramadhani Mwalimu Khamis, Mkurugenzi Mwendeshaji wa ZIC Arafat Haji, wafanyakazi na wadau mbalimbali wa shirika hilo pia walishiriki.

Waziri Saada mbali na kulipongeza shirika hilo kwa mabadiliko hayo, alisema mwonekano mpya wa ZIC unaombatana na maboresho zaidi ya huduma zake, utasaidia kuboresha zaidi imani ya umma juu ya shirika hilo na sekta ya bima kwa ujumla, hatua ambayo itachochea mwamko wa wananchi wengi zaidi katika kutumia huduma za bima.

"Serikali inatambua umuhimu wa sekta ya bima katika maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii yetu. Tunatambua pia kuwa sekta ya bima inachangia katika ukuaji wa uchumi, kupunguza umaskini na kuimarisha usalama wa kifedha kwa wananchi wetu.

"Na hiyo ndio sababu serikali ina nia ya dhati ya kuimarisha ushirikiano wake na wadau wa sekta ya bima hususani wale wanaoonesha nia thabiti ya kujiendesha kwa ustadi mkubwa kama ZIC ili kuleta maendeleo katika sekta hii kupitia utoaji wa huduma bora zaidi kwa wananchi wetu," alisema.

Katika hotuba yake wakati wa tukio hilo muhimu, Haji alielezea hamasa yake kuhusu hatua hiyo muhimu, inatokana na azma thabiti ya ZIC ya kuboresha zaidi mwonekano wake kwa jamii kupitia maboresho ya huduma zake ili kukidhi matakwa ya soko la sasa na kukabiliana na ushindani mkubwa katika sekta ya bima.

"Tunapoimarisha nembo yetu na kubadilisha ofisi zetu, hatulengi tu kubadili mwonekano wetu kuwa wa kisasa, bali pia tulenga kuthibitisha ubora wa huduma zetu ili kuendelea kulinda imani waliyonayo wateja wetu kwetu kama shirika.

"Nembo yetu mpya inawakilisha sifa ya weledi, uaminifu, na mawazo ya ubunifu yenye kuakisi kikamilifu lengo la ZIC la kulinda, kuwezesha na kuhamasisha maendeleo ya watu binafsi na biashara kupitia suluhisho la bima lililoboreshwa," alisema.

Hatua ya shirika hilo imekwenda sambamba na utekelezaji wa programu maalum ya mafunzo kwa wafanyakazi wake ili kuwajengea uwezo wa kwenda sambamba mabadiliko na kasi hiyo mpya inayohusisha ujuzi na weledi kwenye matumizi ya teknolojia katika utoaji huduma za bima.

"Programu hizi za mafunzo zitawajengea wafanyakazi wetu ujuzi na maarifa muhimu ili kuwapa umakini binafsi, kutoa mrejesho wa haraka kwa wateja na kutoa ushauri wa kitaalamu na unaofaa kwa mahitaji ya wateja wetu.

"Zaidi pia ofisi zetu zenye mwonekano mpya zitasaidia kurahisisha mwingiliano na wateja wetu na hivyo kuongeza mvuto na ufanisi wa huduma zetu," aliongeza.




Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum (katikati), akiwa na Mkurugenzi Mwendeshaji wa Shirika la Bima Zanzibar (ZIC), Arafat Haji (kulia) na Balozi wa Bima nchini, Wanu Hafidh Ameir (Mb), wakitazama nembo mpya ya Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) kabla ya uzinduzi rasmi wa nembo hiyo ikiwa ni sehemu ya hatua ya kubadili mwonekano na taswira ya ZIC kijamii na kibiashara Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICGA WETU**

# Wanawake watakiwa kujitosa fursa eneo la bahari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam, Dk. Tumaini Gurumo, amesema ushiriki wa wanawake katika masuala ya bahari siyo mkubwa, kwamba wengi wao wamejikita katika usajili wa usafirishaji wa meli.

Amesema kwenye nafasi ya ubaharia bado idadi ni ndogo na kuna kazi kubwa ya kuhamasisha wanawake kujielekeza katika fani hiyo.

Aliyasema hayo jana visiwani hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari katika maonesho ya biashara ya miaka 60 ya Mapinduzi Zanzibar yanayoendelea Nyamanzi nje ya mji wa Zanzibar.

Gurumo alisema nafasi za ajira baharini hazitazami jinsia na hata sheria za kimataifa zimebadilika na sasa zinampa nafasi mwanamke kuingia baharini na kupata haki zake zinazostahiki sawa na mwanaume.

Alisema mtazamo hasi wa zamani uliyojengeka kuwa mtoto wa kike hawezi kufanya kazi za baharini, kuendelea na mtazamo huo ni kuwazibia fursa, hivyo lazima wanawake kupewa nafasi ili kujikwamua wao na familia zao na taifa kwa ujumla.

Alisema Zanzibar ni kisiwa chenye ajira na nyingi zipo baharini, hivyo ili nchi inapaswa kutoweka mipaka baina ya wasichana na wavulana kuingia katika fani hizo na kusaidia nchi na jamii.

Aidha aliwataka wazazi na walezi kuwapa nafasi wasichana wanaopenda kuingia katika fani hiyo ya bahari ili kuwajengea mustakbali mzuri wa maisha yao ya baadaye.

Akizungumzia changamoto zinazoikabili chuo hicho alizitaja ni upatikanaji wa walimu mabaharia wenye sifa inayohitajika, licha ya chuo hicho kuwa na wataalamu wakiwamo wahandisi, manahodha.

Alisema lakini idadi yao ni ndogo kutokana na uhitaji mkubwa ili kuendana na wingi wa wanafunzi chuoni hapo.

Gurumo alisema pia kuna changamoto ya kuwapatia wanafunzi mafunzo kwa vitendo ndani ya meli zinazosafiri kutoka nchi moja kwenda nyingine badala ya kusoma kwa nadharia darasani.

Alisema chuo hicho kina idadi ya wanafunzi wapatao 4,000 hivyo wanahitaji vijana wengi zaidi kujiunga na chuo kupata mafunzo na kuingia katika utekelezaji wa sera ya uchumi wa buluu.

Alisema upungufu huo wa walimu wa masuala ya bahari unatokana na uchache wa Watanzania waliojikita katika fani hiyo na uchache huo unatokana na awali masomo hayo yakitolewa nje ya nchi.

Gurumo alisema uwepo wa kozi mbalimbali za masuala ya bahari katika chuo hicho, ufumbuzi utapatikana kwa kutengeneza rasilimali nyingi kwa sababu chuo kimeanzisha kozi ambazo zilikuwa hazipatikani hapa nchini.

Hata hivyo alisema uchumi wa buluu wenye tija lazima uzingatie utunzaji wa mazingira ya bahari ili kuendelea kuzalisha rasilimali zinazotegemewa kwa manufaa ya kiuchumi.

# TPA yapongezwa kwa ufanisi bora, yatakiwa isibweteke

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Bandari Tanzania (TPA), imepongezwa kwa utendaji wenye ufanisi, imetakiwa kuongeza juhudi ili kupata mafanikio zaidi.

Pongezi hizo zilitolewa mwishoni mwa wiki na viongozi mbalimbali wa serikali waliotembelea banda la TPA, katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Zanzibar, yaliyofanyika katika viwanja vya Nyamanzi, Zanzibar.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisema sekta ya viwanda na biashara zinaitegemea sana sekta ya uchukuzi katika kufanikisha mipango yake ya kuhudumia wananchi na kuchangia maendeleo ya taifa.

Kigahe alisema bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali na viwanda nchini zinahitaji uhakika wa kupata malighafi na uhakika wa kuyafikia masoko ya ndani na nje ya nchi.

"Tunaipongeza TPA na taasisi nyingine za uchukuzi kwa kazi kubwa ya kuwawezesha Watanzania kupata tija katika shughuli zao za uzalishaji mali na biashara ya mazao na bidhaa zinazozalishwa katika sekta mbalimbali," alisema.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Prof. Godius Kahyarara, aliipongeza TPA kwa kushiriki maonesho yanayoendelea na kwa mafanikio makubwa ya kuhudumia meli na shehena katika nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2023/2024.

"Nimefurahi kwanza kwa kushiriki kwenu katika maonesho haya ambapo tunaungana na Watanzania wenzetu wa upande wa visiwani kutafakari kwa pamoja namna bora ya kuongeza ufanisi wa huduma zetu kwa wananchi na wanufaika wengine," alisema.

Alisema TPA na ZPC zinafanya kazi nzuri katika sekta ya bandari lakini bado ziko fursa za kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na ndiyo maana serikali zote mbili zinafanya jitihada kubwa za kuwezesha ufanisi huo kupatikana.

"Natoa wito kwa Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya TPA kusimamia kikamilifu mipango yenu mliyojiwekea ambayo ikitekelezwa vyema, shughuli za bandari zitakuwa na mchango mkubwa zaidi katika pato la taifa na maendeleo ya nchi yetu kwa ujumla," alisema.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Dk. Ally Possi, alisema ushiriki wa TPA katika maonesho hayo ya Zanzibar ni fursa muhimu ya kukuza ushirikiano kati ya TPA, ZPC na taasisi zingine ili kubadilisha uzoefu na kukutana na wananchi ambao ndio walengwa wakuu wa huduma zinazotolewa na taasisi hizo.

Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa TPA, Nicodemus Mushi, alisema mamlaka hiyo imepata fursa ya kukutana na wananchi wa Tanzania visiwani na kwamba wanaendelea kuwapa elimu kuhusu utendaji wa Bandari Tanzania Bara.

Mushi alisema wamefanikiwa kuwaelimisha wananchi kuhusu mipango ya kuboresha huduma katika eneo la Majahazi katika Bandari ya Dar es Salaam ambalo linahudumia abiria na mizigo inayosafiri kati ya Tanzania Bara na Visiwani.

HABARI KITAIFA

# Barabara mbovu yakwaza

**Na Julieth Mkireri,** VIGWAZA

WAKAZI wa Kijiji cha Kwazokazoka, Kata ya Vigwaza Halmashauri ya Chalinze, wanakabiliwa na kero ya ubovu wa barabara kutoka Kwazoka hadi KItongoji cha Kivungwi.

Pia wana uhitaji wa daraja katika Mto Kiloweko ambao kipindi cha mvua wanafunzi wanahitaji msaada wa kuvushwa na wengine kushindwa kuhudhuria masomo.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Shomari Zinga, akizungumza na Nipashe jana kijijini hapo alisema, kero hiyo ya barabara yenye ukubwa wa kilomita tatu, wamewasilisha kwa Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA).

Alisema ujenzi wa daraja kwenye Mto Kiloweko tathmini iliyofanywa imebaini mahitaji ya Sh. milioni 65 ili kuondoa usumbufu wanaokumbana nao wananchi hususani wanafunzi wakati wa kwenda shule na kurudi nyumbani kipindi cha mvua.

Zinga anasema kwasasa wanaendelea na jitihada za kutafuta wadau wa kuchangia kuwezesha ujenzi wa daraja hilo sambamba na ofisi ya kijiji ambayo tayari wamepata tofali 1,100 kutoka kwa wafadhili.

Diwani wa Vigwaza, Mussa Gama, akizungumzia kuhusu ujenzi wa daraja alisema baada ya tathmini ya TARURA wameanza kusaka wadau wa maendeleo watakao wachangia waweze kuanza ujenzi.

"Eneo hili la mto Kiloweko limekuwa kero kwa wanafunzi wakati mwingine maji yakijaa wanashindwa kwenda shule na kukosa masomo kwa kuwa hakuna mtu anayemudu kuwavusha."

"Halmashauri imetuelekeza tuanze michango ujenzi uanze na wao watamalizia, tumeanza kukutana na wadau wa kwenye kijiji na kata kuwaomba watusaidie," alisema Gama.

Tayari kijiji hicho kimepata mfadhili kwa aliyeahidi kujenga zahanati na kituo kidogo cha polisi vituo vya huduma ambavyo vimekuwa ni mahitaji makubwa katika eneo hilo.



Wanafunzi kutoka vyuo mbalimbali mkoani Shinyanga wakijitokeza kuchangia damu katika Kituo cha Afya Kambarage ili kuokoa maisha ya mama na mtoto wakati wa kujifungua, walichangia uniti 25 za damu mwishoni mwa wiki. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Ndoa za serikali zimesajiliwa - RITA

**Na Mary geofrey**

WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), imesema wanandoa wenye vyeti vya ndoa vya serikali, zimesajiliwa na hawana sababu ya kuzisajili tena.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini Dar es Salaam, Ofisa Mtendaji Mkuu wa RITA, Frank Kanyusi, alisema kuwa wanandoa wenye vyeti vya ndoa vya serikali zinatambuliwa na sheria.

"Napenda ieleweke kwamba wanandoa ambao wamefunga ndoa za kidini, kiserikali au kimila na kupewa vyeti vya ndoa vya serikali, ndoa zao zimesajiliwa kwa mujibu wa sheria. Wananchi waepuke uzushi unaoendelea kuwa hazijasajiliwa," alisisitiza.

Kanyusi alirejea Sheria ya Ndoa, Sura ya 29 kifungu cha 30, 43 na 46 na kueleza kuwa RITA ina taarifa zote za ndoa ambazo wanandoa wamepewa vyeti vya ndoa vya serikali.

"Msajili Mkuu inaweza kutoa nakala nyingine endapo wanandoa watapoteza vyeti walivyopewa awali na wafungishaji ndoa," alisisitiza.

Aidha, aliwataka wafungishaji ndoa kusajili kwenye mfumo wa RITA wa kielektroniki kupitia eRITA kwasababu wanaweza kupata huduma hiyo popote nchini.

Aliwataka kuhuisha leseni zao za kufungisha ndoa kwa wakati na wahakikishe wanasajili ndoa zote zinapofungwa, kuwapa wanandoa vyeti na kufanya marejesho ya ndoa walizofunga kila mwezi ili Msajili Mkuu awe na taarifa au rekodi zote kwa wakati.

Kanyusi alisema RITA imeweka mkazo kwenye kuwasajili watoto wote wenye umri wa chini ya miaka mitano nchi nzima chini ya mpango maalumu wa kuwasajili watoto katika ofisi za kata na kliniki za mama na mtoto.

Aidha, alisema kumekuwapo changamoto ya ukubalifu wa vyeti katika baadhi ya taasisi za umma na binafsi na wananchi kupata usumbufu.

"Napenda ieleweke kwamba vyeti vilivyojazwa na mkono vina uhalali sawa na vyeti vingine vinavyotolewa na kompyuta hivyo vinafaa kwa matumizi yote...RITA ndiye mwenye dhamana na mamlaka ya kutoa vyeti vya kuzaliwa ikiwa ni pamoja na kuvihakiki. Iwapo kuna mashaka yoyote juu ya vyeti vyote vinavyotolewa na ofisi yetu nawaomba muwasiliane nasi kwa ajili ya ufafanuzi, uhakiki pamoja na kuthibitisha uhalali wa nyaraka hizo," alisema Kanyusi.

## Spika Tulia asifu benki kuchochea maendeleo

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SPIKA wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Ackson na Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zubeir Ali Maulid, wamesema mchango wa Benki ya NMB kwa maendeleo ya taifa unaakisi ukubwa na uimara wa taasisi hiyo.

Viongozi hao pia wameitaka benki hiyo kudumisha ushirikiano na mihimili hiyo ya dola pamoja na serikali za pande zote za Muungano.

Dk. Tulia ambaye ni Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) na Maulid wametoa kauli hizo wakati wa hafla ya usiku wa tuzo kwa washindi na mabingwa wa bonanza lililoshirikisha timu za wafanyakazi wa NMB na wabunge na wawakilishi lililofanyika mwishoni mwa wiki, ikiwa ni sehemu ya sherehe za Miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Akitoa neno la shukrani kwa kudhamini bonanza hilo, Dk. Tulia alipongeza NMB kwa namna inavyotumia vyema fungu la Programu ya Uwajibikaji kwa Jamii (CSR), ambako imezisapoti pakubwa serikali zote mbili kupambana na changamoto zinazokwaza ustawi wa sekta za elimu, afya, majanga na mazingira.

"Nitumie fursa hii kuwashukuru sana NMB, kwa ushirikiano mkubwa walioonesha kwa Baraza la Wawakilishi kufanikisha bonanza hili, ambalo limegharimu kiasi kikubwa cha fedha.

"Hapa tumesikia kitu kisicho cha kawaida, mbunge kutoka chama kisicho cha Mapinduzi, akisifia kazi nzuri inayofanywa na Dk. Mwinyi na Dk. Samia, maana yake ni kuwa kazi za marais hawa wawili zimepitiliza, hata usipotaka kuziona utaziona tu," alisema Dk. Tulia.

Akimkaribisha Spika Tulia kuzungumza, Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zubeir Ali Maulid, alisisitiza umuhimu wa NMB kudumisha ushirikiano na serikali za pande zote mbili za Muungano, pamoja na mabunge, kwa kuwa kufanya hivyo ni moja ya kudumisha na kustawisha Muungano ulioasisiwa na waanzilishi wake marais wa kwanza wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Ofisa Mkuu wa Fedha wa NMB, Juma Kimori, alilishukuru Baraza la Wawakilishi, Spika na wajumbe wake kwa kuichagua NMB kushirikiana nao katika kufanikisha bonanza hilo na kusisitiza kwamba taasisi yake ikiwa ni mdau namba moja wa serikali zote mbili, itaendeleza ushirikiano uliopo kwa kuwa wanajali na kuthamini ushirikiano huo.

"Binafsi niseme nimefarijika sana kwa aina ya ushirikiano uliopo baina ya Bunge la Tanzania na Baraza la Wawakilishi, nasi tumefanya makubwa kila upande," alisema Kimori aliyemwakilisha Ofisa Mtendaji Mkuu wake Ruth Zaipuna.

# UN: Hali inatisha Ukanda wa Gaza

**GAZA,** Palestina

MRATIBU wa misaada ya dharura wa Umoja wa Mataifa (UN), Martin Griffiths, amesema hali katika Ukanda wa Gaza ni ya kutisha kutokana na mashambulizi ya Israel yanayoendelea katika eneo hilo, huku akitoa wito wa kusitisha vita hivyo kutokana na kwamba vinaathiri zaidi raia.

Aidha, wakati UN ikitoa wito huo, maofisa wa Wizara ya Afya inayoongozwa na Hamas, walibainisha kuwa ndani ya saa 24 zilizopita Israel ilifanya mashambulizi katika mji wa Kusini mwa Gaza na kuua raia 135. Na kwamba zaidi ya wananchi milioni moja wanaoishi katika eneo hilo ni wale waliokimbia makazi yao kwa hofu ya vita.

Akizungumza mbele ya Baraza la Usalama la UN kuhusu hali ya kiutu nchini Israel na Palestina, Griffiths alisema kwa siku 100 za vita tangu Oktoba 7, 2023 watu 23,000 wameuawa na 58,000 wamejeruhiwa. Zikiwa ni takwimu alizozinukuu kutoka Wizara ya Afya ya Gaza na kwamba asilimia 70 ya waliouawa ni wanawake na watoto.

**Taarifa ilibainisha kuwa Ujerumani ilifanya mauaji ya halaiki ya kwanza ya karne ya 20 nchini Namibia kati ya 1904 na 1908.**

Kiongozi huyo anayeshughulikia masuala ya kibinaadamu UN, alisema kuwa watu milioni 1.9 ambao ni asilimia 85 ya idadi jumla ya wakazi wa Gaza wamelazimika kuyahama makazi yao kutokana na mashambulizi mfululizo yanayofanywa na Israel yakielekezwa kwa raia.

"Hali ya mfumo wa afya inazidi kuzorota, huduma za kiutu zimekwama pakubwa na wafanyakazi 148 wa UN na mashirika ya kiraia wameuawa. Pia ofisi karibu 134 za Shirika la Umoja wa Mataifa linalowahudumia wakimbizi wa Palestina (UNRWA) zimeshambuliwa," alisema Griffiths.

**MAREKANI**

Katika hatua nyingine, maofisa wawili wa Marekani walibainisha kuwa nchi hiyo ilifanya mashambulizi mapya dhidi ya waasi wa Houthi wa nchini Yemen na kulenga eneo linalozingatiwa kuwa tishio kwa meli za kibiashara katika Bahari ya Shamu.

Hivi karibuni waasi wa Kihouthi walianzisha mashambulizi kadhaa ya makombora na ndege zisizo na rubani dhidi ya meli katika Bahari ya Shamu ikiwa ni majibu kwa operesheni ya kijeshi ya Israel katika Ukanda wa Gaza dhidi ya kundi la Hamas.

Ilielezwa kuwa mashambulizi hayo yalifanywa baada ya mengine 30 ya awali yaliyokuwa yamelenga kupunguza uwezo wa Wahouthi wa kuitishia njia ya kibiashara katika Bahari ya Shamu.

Kwa mujibu wa maofisa hao wa Marekani ambao hawakutaka majina yao kutajwa, miundombinu iliyolengwa katika mashambulizi hayo ni pamoja na vituo vya kuhifadhi vifaa, mifumo ya anga na maghala ya silaha.

Naibu Mkuu wa Shirika la Habari la Wa Houthi, Nasreddin Amer, alibainisha kuwa mashambulizi hayo yaliyofanyika dhidi yao hayakusababisha majeruhi wala hasara ya mali. Akisisitiza kuwa Marekani itawajibika kwa hilo, na watajibu mashambulizi haraka iwezekanavyo.

**NAMIBIA**

Kwa upande mwingine, Rais wa Namibia, Hage Geingob, ameikosoa Ujerumani kwa kuunga mkono Israel katika kesi ya mauaji ya halaiki huko Ukanda wa Gaza katika Mahakama ya Kimataifa ya Haki (ICJ) iliyowasilishwa na Afrika Kusini.

"Ujerumani imechagua kutetea Israel katika ICJ kuhusu vitendo vya mauaji ya halaiki na vya kutisha vya serikali ya Israel dhidi ya raia wasio na hatia huko Gaza na maeneo ya Palestina yanayokaliwa kwa mabavu. Hakuna binadamu mpenda amani anayeweza kupuuza mauaji yanayofanywa dhidi ya Wapalestina huko Ukanda wa Gaza," alisema Rais Geingob.

Taarifa ilibainisha kuwa Ujerumani ilifanya mauaji ya halaiki ya kwanza ya karne ya 20 nchini Namibia kati ya 1904 na 1908, na kwamba maelfu ya Wanamibia wasio na hatia walikufa chini ya hali ya kikatili ya ukoloni. **DW, BBC**



Uharibifu uliosababishwa na mashambulizi ya anga ya Israel katika Ukanda wa Gaza. **PICHA: MTANDAO**

## Sintofahamu mgomo wakulima Ujerumani

**BERLIN,** Ujerumani

KANSELA wa Ujerumani, Olaf Scholz, ametoa wito wa kuwapo utulivu na utayari wa kukubali maafikiano wakati nchi hiyo ikikabiliwa na maandamano ya wakulima wenye hasira kuhusu mpango wa kupunguza ruzuku yao ya mafuta.

Kiongozi huo alito wito huo jana huku akionya kuhusu watu wenye itikadi kali wanaochochea hasira miongoni mwa umma.

Inaelezwa kuwa wakulima walifunga barabara kuu na kuvuruga usafiri kote nchini humo kwa kutumia matrekta yao kama sehemu ya wiki ya maandamano ya kupinga mpango wa kuondoa ukomo wa kodi ya dizeli inayotumika katika kilimo.

Hata hivyo Kansela Scholz alisema kuwa serikali ilizichukua kwa umakini hoja za wakulima na kusisitiza kuwa ilifikia maelewano mazuri, japokuwa wakulima wanaendelea kusisitiza kuhusu kubatilishwa kikamilifu kwa mpango wa kupunguzwa kwa ruzuku.

"Maofisa watajadili nini kingine wanaweza kukifanya ili kuhakikisha sekta ya kilimo inakuwa na mustakabali mwema," alisema Scholz. **DW**

## Dangote kuanza kazi Nigeria

**LAGOS,** Nigeria

KAMPUNI ya kusafisha mafuta ya Dangote ya Nigeria imeanza kusafisha dizeli pamoja na mafuta ya ndege, baada ya ucheleweshwaji wa muda mrefu wa ujenzi kwenye kiwanda hicho chenye uwezo wa kuzalisha mapipa 650,000 kwa siku.

Kwa mujibu wa shirika la habari la Reuters, kiwanda hicho ndicho kikubwa zaidi barani Afrika, kilichojengwa kwenye Peninsula iliyopo nje ya mji mkuu wa kibiashara wa Lagos, kwa gharama ya dola bilioni 20, (zaidi ya Sh. Trilioni 49.6) ambacho kinamilikiwa na Aliko Dangote.

Inaelezwa kuwa ingawa Nigeria ndiye mzalishaji wa juu wa mafuta barani Afrika, imekuwa ikitegemea mafuta kutoka mataifa ya nje. Na kwamba kiwanda cha Dangote sasa kitaiwezesha Nigeria siyo tu kujitegemea, bali pia kuuza mafuta kwenye mataifa jirani ya Afrika Magharibi.

Hata hivyo ilielezwa kuwa kampuni hiyo itakuwa chachu ya kubadili biashara ya mafuta katika ukanda wa Atlantiki.

Maofisa wa kampuni hiyo waliambia Reuters kwamba kitaanza majaribio ya wiki hii, baada ya kupokea shehena ya sita ya mafuta ghafi Januari 8, mwaka huu. **VOA**

# KILIMANJARO PREMIUM LAGER YATOA WITO KWA WASHIRIKI MARATHON 2024

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU ukiwa umebaki takriban mwezi mmoja kabla ya mbio maarufu za Kilimanjaro International Marathon 2024 kufanyika Mjini Moshi, mdhamini mkuu wa mbio hizo, Kilimanjaro Premium Lager, ametoa wito kwa washiriki wote kukamilisha maandalizi kwa kuwa siku zimebaki chache.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Meneja wa chapa ya Kilimanjaro Premium Lager, Catherine Lyakurwa, alisema siku zimebaki chache hivyo washiriki hasa wale wa mbio za Km 42 hawana budi kujiandaa vizuri.**

"Hii ni mbio ndefu ambayo inahitaji mshiriki ajiandae vizuri. Tunafahamu kuwa washiriki wamekuwa wakifanya mazoezi na sasa tuna takriban mwezi mmoja tu ni vizuri tukamilishe maandalizi mapema tayari kwa mbio hizi," alisema.

Alisema mbio za Km 42 zimejizolea umaarufu mkubwa siku za hivi karibuni huku washiriki wakiongezeka mwaka hadi mwaka."Namba za kukimbilia zinakaribia kuisha kwa hiyo natoa wito kwa wale ambao hawajajisajili wafanye hivyo mara moja kwani zoezi litafungwa mara tu nafasi zitapojaa," alisema.

Alisema Bia ya Kilimanjaro Premium Lager itaendelea kufanya kazi kwa karibu na wadhamini wenza na waandaaji ili kuhakikisha mbio za mwaka huu zinafanikiwa na kuacha kumbukumbu ya aina yake. "Tumekuwa wadhamini wa mbio hizi tangu kuanzishwa kwake miaka 22 iliyopita kutokana na mbio hizi kuwa na faida kubwa kwa biashara yetu na kwa nchi kwa ujumla," alisema.

Meneja huyo pia alitoa wito kwa wadhamini wenza kujiandaa na changamoto ya washirika ambapo wadhamini mbalimbali huandikisha washiriki wao katika mbio mbalimbali kisha waandaaji hutumia wastani wa muda wao kumaliza mbio ili kubaini mshindi wa kwanza, wa pili na wa tatu.

Aliwashukuru wadhamini wenza kwa ushirikiano mkubwa kwani bila ushirikiano kati ya wadhamini na waandaaji mbio hizo zisingekuwa na mafanikio makubwa.

Katika hatua nyingine, waandaaji wa mbio hizo wamesema kufunga usajili mapema kunasaidia katika maandalizi kama inavyotakiwa na Chama cha Riadha Duniani (WA) ili kuhakikisha usalama wa washiriki na kwamba waandaaji wanaweza kuandaa mahitaji muhimu kama maji na matunda kwa wakati.

Wadhamini wa tukio la mwaka huu ni Kilimanjaro Premium Lager- Km 42, Tigo- Km 21(Half Marathon), Gee Soseji - Km 5 (Fun Run). Wadhamini wa meza za maji ni Simba Cement, Kilimanjaro Water, TPC Sugar, TotalEnergies na CRDB Bank. Wabia rasmi ni KiliMedair, Garda World Security, CMC Automobiles, Sal Salinero Hotel na wasambazaji wakuu ni Kibo Palace Hotel na Keys Hotel.

Mbio za mwaka huu zitafanyika Februari 25 katika Chuo Kikuu Cha Ushirika Moshi.

Kilimanjaro Premium Lager Marathon huandaliwa na Kilimanjaro Marathon Company Limited na kuratibiwa kitaifa na Kampuni ya Executive Solutions Limited.

# Kocha Mlandege: Tulistahili ubingwa

**Na Faustine Feliciane,** ZANZIBAR

KOCHA wa Mabingwa wa Kombe la Mapinduzi, Hassan Ramadhan, amesema timu yake ilistahili kutwaa ubingwa huo kutokana na aina ya soka wanalolicheza.

Ramadhan alisema kikosi chake ndicho kikosi bora cha mashindano hayo kwa sababu tangu kuanza kwa michuano hiyo Desemba 28, mwaka jana wameruhusu magoli mawili pekee.

Alisema walipofanikiwa kuingia fainali walikuwa na uhakika wa kutwaa ubingwa huo kwa sababu aliona udhaifu wa Simba na akajua watapata ushindi na kuwashangaza wapinzani wao.

"Simba tuliiona, tuliona ubora wao na udhaifu wao, wanacheza mpira wa pasi nyingi, lakini hawana mbinu ya kupenya kwenye safu ya ulinzi nzuri kama yetu, tuliwaacha wacheze mpira wao na sisi tulikuwa na mahesabu yetu ambayo yamefanikiwa," alisema Ramadhan.

Alisema aliwaambia wachezaji wake wacheze kwa mahesabu na kufanya mashambulizi ya kushtukiza kwa sababu ya udhaifu wa wapinzani wao walijua watapata goli.

"Safu yao ya ulinzi niliona ina mapungufu, nikawataka wachezaji wangu wajilinde sana na kufanya mashambulizi ya kushtukiza hasa wachezaji wa simba wanakuwa wamesogea juu, na kweli umetulipa tukapata ushindi huu muhimu na kutwaa ubingwa," alisema Ramadhan.

Aidha, alisema Simba wanatimu nzuri, lakini lazima wafanyia kazi mapungufu yao kwa sababu wanaiwakilisha nchi kwenye mashindano ya kimataifa.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kulia), akikabidhi jezi ya mchezaji wa zamani wa Taifa Stars, Leodgar Tenga, kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya TCB, Adam Mihayo, aliyoinunua kwa Sh. milioni saba wakati wa harambee kwa wadau wa michezo kuchangia timu za taifa nchini, iliyofanyika wiki iliyopita jijini Dar es Salaam. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# CRDB yapeleka Watanzania kushuhudia AFCON

**Na Mwandishi Wetu**

WATEJA wanne wa Benki ya CRDB, akiwamo Mbunge wa Morogoro Kusini, Hamisi Taletale pamoja na wengine watatu, wameondoka kuelekea Ivory Coast kushuhudia michuano ya Mataifa ya Afrika (AFCON) iliyoanza juzi usiku.

Washindi hao walipatikana kwenye droo mbili za Kampeni ya 'Tisha na Tembocard Tukakiwashe AFCON' zilizochezeshwa kati ya tatu zilizopangwa kufanyika mpaka mwishoni mwa mwezi huu. Kampeni hiyo inayohamasisha matumizi ya kadi katika kufanya malipo, inatekelezwa na Benki ya CRDB kwa kushirikiana na Kampuni ya Visa.

Mbali na mbunge huyo wa Morogoro Kusini, wateja wengine walioagwa na benki hiyo kwenda Ivory Coast ni Evelyne Rwebugisa, Josephine Marealle na Dickson Kabaka wa jijini Dar es Salaam.

Akiwaaga wateja hao waliobahatika, Mkuu wa Idara ya Huduma za Kadi wa Benki ya CRDB, Farid Seif, alisema kwa miaka mingi taasisi hiyo kubwa ya fedha nchini imekuwa inaongoza kwa kutoa ufumbuzi wa changamoto zilizopo kwenye huduma za benki kwa kubuni namna ya kuwafikia wananchi na kukidhi mahitaji yao kwa wakati.

"Leo tunawaaga wateja wanne, hivyo tunabakiwa na nafasi nne nyingine za wateja watakaotumia sana kadi zao kufanya miamala kuanzia kulipia huduma au bidhaa wanazonunua mtandaoni, maduka makubwa, vituo vya mafuta au namna nyingine yoyote.

"Benki ya CRDB imeona ipo haja ya kuwapa nafasi wateja wake kwenda kuungana na familia kubwa ya soka barani Afrika," alisema Seif.

Alisema mpira wa miguu ni miongoni mwa michezo inayopendwa zaidi nchini na duniani kwa ujumla na AFCON ndio michuano mikubwa barani Afrika, hivyo Benki ya CRDB iliona ni vema ikatoa nafasi chache kwa wateja wake kwenda kushuhudia mtanange wa mataifa yaliyofuzu mwaka huu.

Akizungumza kwenye hafla hiyo ya kuagwa, Mbunge Taletale, maarufu Babu Tale, alipongeza Benki ya CRDB kwa kutoa nafasi hiyo kwa wateja wake na akashauri taarifa ziwafikie Watanzania wengi zaidi ili kila mmoja ajaribu bahati yake.

"Nilipopigiwa simu kuwa nimeshinda safari, kwanza sikuamini. Nilidhani ni matapeli wa mtandaoni, lakini nilipofuatilia nilijiridhisha kwani droo huchezeshwa na kurushwa mbashara kwenye mitandao ya kijamii ya Benki ya CRDB. Nimefurahi sana kupata nafasi hii na ningetamani kuona Watanzania wengi zaidi wananufaika nayo," alisema Taletale.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### HENDERSON AKARIBIA AJAX

AJAX wanaamini wanakaribia kukamilisha mkataba wa mkopo kwa kiungo wa kati wa England, Jordan Henderson mwenye umri wa miaka 33, kutoka Al-Ettifaq ya Saudia. ***(Mirror)***

#### JUVE NAO KWA AL-ETTIFAQ

KLABU ya Juventus pia inavutiwa na Jordan Henderson na wana matumaini ya kumsaini nahodha huyo wa zamani wa Liverpool kwa mkataba wa awali wa miezi sita na chaguo la kufanya uhamisho huo kuwa wa kudumu kutoka Al-Ettifaq ya Saudia. ***(Gazzetto dello Sport)***

#### NEVES AWANIWA UNITED

MANCHESTER United wanatumaini kuanzisha mazungumzo na Benfica kuhusu mkataba wa majira ya joto kwa kiungo wa kati wa Ureno, Joao Neves mwenye umri wa miaka 19. ***(Mirror)***

#### MEJBRI AWINDWA SEVILLA

KLABU ya Sevilla bado ina matumaini ya kumsajili kiungo wa kati wa Tunisia, Hannibal Mejbri kwa mkopo, ingawa Manchester United wangependelea mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 ajiunge na Everto. ***(Revolo)***

#### SOYUNCU ATAKIWA FULHAM

FULHAM wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa FC Porto kuwania saini ya mlinzi wa Uturuki na Atletico Madrid mwenye umri wa miaka 27, Caglar Soyuncu. ***(A Bola via Sport Witness)***

#### MANGALA ATAJWA NAPOLI

JUVENTUS imeungana na Napoli na Galatasaray katika juhudi za kumwania kiungo wa kati wa Nottingham Forest na Ubelgiji, Orel Mangala kwa mkopo. ***(Sky Germany)***

#### MUNOZ ANUKIA PALACE

KLABU ya Crystal Palace wanatumaini kukamilisha dili la pauni milioni 10 kwa beki wa kulia wa Genk, Daniel Munoz raia wa Colombia mwenye umri wa miaka 27. ***(Sun)***

#### MEJIA SAFI SEVILLA

KLABU ya Sevilla imekubali mkataba wa kumsajili mshambuliaji wa Manchester United mwenye umri wa miaka 20, kutoka Colombia, Mateo Mejia kwa mkataba wa kudumu. ***(Fabrizio Romano)***

#### BESIKTAS: KILISCOY HAUZWI

KLABU ya Besiktas imekataa ofa kutoka kwa Wolves kwa ajili ya mshambuliaji wao mwenye umri chini ya miaka 19, Mturuki Semih Kılıcsoy. ***(Haberturk)***

#### LINGARD ATIMUA WAKALA

JESSE Lingard amemfuta kazi wakala wake huku mshambuliaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 31, akiendelea kutafuta klabu mpya baada ya kuachwa na Nottingham Forest. ***(Sky Sports)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA: DE BRUYNE NI GWIJI HAPA MAN CITY

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amemsifu Kevin De Bruyne kama "gwiji" baada ya kiungo huyo kufunga bao na kutoa asisti wakati akirejea kwenye Ligi Kuu England na kuisaidia Manchester City kushinda mabao 3-2 dhidi ya Newcastle United.

**De Bruyne aliingia kama mchezaji wa akiba dakika ya 69 wakati City wakiwa nyuma kwa mabao 2-1 pale kwenye Uwanja wa St James' Park kabla ya kufunga na kufanya 2-2 na kisha kumtengenezea Oscar Bobb mwenye umri wa miaka 20 kufunga bao la ushindi dakika ya 91.**

Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Mbelgiji huyo kucheza kwenye ligi tangu Agosti mwaka jana baada ya kukaa nje ya uwanja kwa miezi mitano kwa sababu ya jeraha la misuli ya paja ambalo lilihitaji upasuaji.

> ●●● Bao na asisti, anapendwa na watu wetu na tunatumai katika miezi ya hivi karibuni...

"Yeye ni gwiji," alisema Guardiola. "Nilihisi hayuko tayari kwa dakika 90 baada ya miezi mitano kwa hiyo tuna hali hiyo.

"Bao na asisti, anapendwa na watu wetu na tunatumai katika miezi ya hivi karibuni anaweza kutusaidia kuwa hapo hadi mwisho."

Matokeo hayo, ambayo yalionekana kutowezekana pale Alexander Isak na Anthony Gordon walipofunga katika muda wa dakika mbili za kipindi cha kwanza na kuifanya Newcastle kuwa mbele kwa mabao 2-1 baada ya bao la kwanza la Bernardo Silva, yanaifanya City kupanda hadi nafasi ya pili kwenye msimamo, pointi mbili nyuma ya vinara Liverpool.

Na baada ya jioni ya kufurahisha, Guardiola alijisikia ujasiri kuzungumza juu ya uwezekano wa timu yake kushinda taji la nne la Ligi Kuu England kwa mara ya nne mfululizo.

"Timu iko hai," alisema.

"Kwa nini tusijaribu tena? Tulishinda mataji matatu mfululizo, kwa nini isiwe hivyo? Ni muhimu sana kwa sababu Liverpool walisafiri kwa ndege mwezi uliopita na lazima tuende Anfield kwa hiyo ni bora kuwa karibu nao."

Hasara moja kwa City ilikuwa jeraha kwa Ederson ambalo lilimlazimu mlinda mlango huyo wa Brazil kutoka uwanjani ndani ya dakika tano.

Timu ya Guardiola haitacheza tena hadi mechi yao ya raundi ya nne ya Kombe la FA dhidi ya Tottenham Hotspur Januari 26, na Guardiola anatumaini kuwa tatizo si kubwa.

# POCHETTINO: HATUHITAJI MSHAMBULIAJI CHELSEA



**LONDON,** England

MAURICIO Pochettino amepuuza mapendekezo wanayoamini kuwa Chelsea inahitaji kusajili mshambuliaji Januari hii na kupuuzia uvumi wa kutaka kumnunua fowadi wa Brighton, Evan Ferguson.

Chelsea wametatizika kutafuta mabao msimu mzima na hawakuwa na Christopher Nkunku na Nicolas Jackson wakati wakiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Fulham Jumamosi kwenye Uwanja wa Stamford Bridge.

Pochettino alisema Ijumaa kwamba “tutaona hali ilivyo” baada ya kukiri wasiwasi wake kutokana na kudorora kwa hivi punde zaidi kwa Nkunku.

Mchezaji huyo aliyenunuliwa kwa pauni milioni 52 kutoka RB Leipzig majira ya joto, ameichezea klabu hiyo mara nne pekee baada ya kupata jeraha baya la goti wakati wa maandalizi ya msimu mpya.

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba Chelsea inavutiwa na Victor Osimhen wa Napoli na Ivan Toney wa Brentford, lakini uwezekano wa kuwasajili Januari hii ni mdogo.

Santiago Gimenez wa Feyenoord ni chaguo jingine, lakini alipoulizwa haswa kuhusu nia kwa Ferguson, Pochettino alisema: “Hapana, nadhani unajua vizuri sizungumzi kuhusu uvumi.

“Sitazungumza kamwe kuhusu wachezaji ambao wako katika klabu tofauti, naheshimika sana hapana hatuongei tunapima kikosi na ikitokea kitu tutawasiliana, lakini kwa sasa hatukuchukua maamuzi yoyote.

“Sijawahi kusema tunahitaji mshambuliaji wa kati. Hapana, kwa sababu baada ya hapo tunatengeneza tatizo, mimi na watu wangu. Sikuwahi kusema hivyo. Sikusema hivyo jana katika mkutano wangu na waandishi wa habari kwamba tunahitaji mshambuliaji.

## Eriksson: Nimebakisha mwaka 1 kuishi

**STOCKHOLM,** Sweden


KOCHA wa zamani wa England, Sven-Goran Eriksson, amesema amebakisha mwaka mmoja kuishi baada ya kugundulika kuwa na saratani isiyotibika.

Eriksson mwenye umri wa miaka 75, alikuwa kocha wa kwanza wa kigeni kuinoa England na aliiongoza nchi hiyo kufika robo fainali za Kombe la Dunia 2002 na 2006 na michuano ya Euro 2004.

“Ukipata meseji kama hiyo, unathamini kila siku na unafurahi unapoamka asubuhi na unajihisi sawa, kwa hiyo ndicho ninachofanya,” alisema Eriksson akikiambia Kipindi cha BBC World Sporting Witness.

Eriksson, ambaye amefundisha kabumbu kwa miaka 42, aligundulika kuwa na saratani mwaka mmoja uliopita na aliacha majukumu yake ya hivi karibuni ya ukurugenzi wa michezo katika klabu ya Karlstad ya Sweden miezi 11 iliyopita kutokana masuala ya afya.

Klabu alizofundisha ni pamoja na Degerfors na Gothenburg za Sweden, Benfica ya Ureno, AS Roma, Fiorentina, Sampdoria na Lazio za Italia na akitwaa mataji kadhaa.





# Ivory Coast watetema Afcon

**ABIDJAN,** Ivory Coast

WENYEJI Ivory Coast walifungua kampeni yao ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon), kwa ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Guinea-Bissau, juzi.

Seko Fofana na Jean-Philippe Krasso walifunga katika kila kipindi kwa wenyeji hao walipokamilisha ushindi wa mabao 2-0 wa Kundi A dhidi ya Guinea-Bissau katika mchezo wa Kombe la Mataifa ya Afrika.

Fofana alikaribia kufunga bao la kuongoza mara mbili kabla ya muda wa mapumziko, lakini juhudi nyingine kali zilifanywa na Ouparine Djoco.

Krasso alifunga bao la pili baada ya kipindi cha mapumziko kutokana na kudhibiti kwa akili chini ya shinikizo kwenye eneo la goli.

Fainali za Afcon za 2023 zimerudishwa nyuma kwa miezi sita - mapema 2024 - ili kuepusha msimu wa mvua huko Afrika Magharibi, lakini kuchelewa kulisaidia Ivory Coast kukamilisha maandalizi yao, na gharama ya jumla ya kuandaa zaidi ya bilioni moja.

Ivory Coast wanatafuta kushinda taji hilo kwa mara ya tatu baada ya kushinda mwaka wa 1992 na 2015, na ilibidi waanze harakati zao za kutafuta ubingwa bila mshambuliaji chaguo la kwanza, Sebastien Haller kwa sababu ya jeraha.

Wenyeji Ivory Coast walikuwa wakipewa nafasi kubwa dhidi ya timu ya Guinea-Bissau ambayo sasa haijashinda mechi yoyote kati ya 10 za fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika, huku wachezaji kadhaa wakikosekana kutokana na majeraha, watafurahi kuwa wameanza kampeni zao kwa matokeo chanya mbele ya watazamaji 60,000.

Ivory Coast watacheza tena Alhamisi watakapomenyana na Nigeria katika mchuano mkubwa zaidi katika kundi hilo, huku Guinea-Bissau wakichuana na Equatorial Guinea siku hiyo.

Mechi hizo zitachezwa tena katika Uwanja wa Abidjan wa Alassane Ouattara.

HABARI MICHEZO

# SPORTPESA SASA YAJA NA 'AFCON USHINDI NI SPORTPESA'

Na Mwandishi Wetu

KAMPUNI namba moja ya Michezo ya Kubashiri, SportPesa imezindua kampeni iitwayo "Afcon Ushindi ni SportPesa" ambayo ni maalum kwa ajili ya wateja wake kujishindia zawadi ya shilingi 5,000 kwa watu 100 kila siku, na simu janja kwa watu watatu kila wiki.

Promosheni hiyo itawapa fursa wapenzi wote wa michezo, wateja wapya na wanaoendelea kubashiri na SportPesa kuingia kwenye droo baada ya kujisajili na kuweka fedha kwenye akaunti zao za SportPesa na kisha kubashiri.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano SportPesa, Sabrina Msuya, akizungumza wakati wa uzinduzi wa promosheni hiyo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, alisema promosheni hiyo itadumu kwa siku 30.

"Promosheni hii inampa nafasi kila wa mteja wa SportPesa kujishindia zawadi hata kama atakosa matokeo ya bashiri zake, mteja akishaweka pesa kwenye akaunti yake ya SportPesa na kuweka bashiri yake moja kwa moja ataingia kwenye droo ya wiki.

"Wateja wetu wanafursa ya kujishindia zawadi za kila siku Sh. 5,000, kwa upande wa zawadi za wiki, washindi watatu watajinyakulia simu janja.

"Pia wateja wetu wanaweza kuweka bashiri kwenye matukio ya michezo ya ndani na nje ya nchi kupitia tovuti ya SportPesa, USSD, SMS, au APP," alisema Sabrina.

Sabrina alisema promosheni hiyo iliyoanza rasmi Januari 13 itadumu hadi Februari 11, mwaka huu.

# Wanamaji FC watwaa ubingwa Umoja Cup 2023

Na Mwandishi Wetu

TIMU ya Wanamaji FC wametawazwa kuwa mabingwa michuano ya Umoja Cup 2023 baada ya kuichapa Shirati Mji FC bao 1-0 katika mchezo wa fainali uliopigwa hivi karibuni katika Uwanja wa Maji Shirati Sota wilayani Rorya.

Katika mechi hiyo iliyokuwa kali na yakusisimua huku ikihudhuriwa na umati wa watu wilayani humo, Wanamaji FC walipata ushindi huo katika dakika ya 29 kupitia kwa Nicolas Antony baada ya kupokea pasi murua kutoka kwa Riziki Abega.

Bao hilo lilidumu hadi dakika ya mwisho licha ya jitihada Za Shirati Mji FC kwani ngome ya ulinzi ya Wanamaji ilikuwa imara kwa dakika zote 90.

Mgeni rasmi katika mchezo huo wa fainali alikuwa Ofisa Michezo wa Mkoa wa Mara, Makondo Makondo, huku pia ukihudhuriwa na mdhamini wa Umoja Cup Rorya, Peter Owino.

Akikabidhi zawadi kwa washindi Ofisa Michezo wa Mkoa wa Mara, Makondo alisisitiza umuhimu wa wadau wa michezo kujitokeza wilayani hapo na mkoa wa Mara kwa ujumla ili kusaidiana na Owino kuinua vipaji vya soka.

"Tumsaidie Peter Owino ili mashindano haya yanayokuwa kila mwaka yazidi kuimarika," alisema.

Kwa kutwaa ubingwa huo Wanamaji waliibuka na kombe pamoja na Sh. 500,000, wakati Shirati Mji FC ikiondoka na Sh.150,000 na seti moja ya jezi kwa kumaliza nafasi ya pili huku tuzo ya heshima ikienda kwa, Christopher Owinjo Nyatega.



Kikosi cha Wanamaji FC, kilichotwaa ubingwa wa Umoja Cup Rorya 2023. MPIGAPICHA WETU

# *Benchikha ataka straika wa mabao*

INATOKA UKURASA 24

mpira hasa kipindi cha pili.

"Ni ngumu sana kucheza na timu ambayo wachezaji wao wote wanarudi nyuma na kujazana golini kwao, tulikuwa na wakati mgumu na kujikuta tunapoteza mchezo," alisema Banchikha na kuongeza,

"Nawapongeza Mlandege kwa kuchukua ubingwa, mashindano yalikuwa mazuri na yametusaidia sana sisi makocha katika kuvijenga vikosi vyetu, yametusaidia kuona wapi tunapaswa kurekebisha," alisema Benchikha.

Alisema kwa sasa wanarejea kwenye uwanja wa mazoezi kujiandaa na michezo ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na michezo ya Kombe la FA.

# Yanga yatamba kupata jembe

INATOKA UKURASA 24

kipya kuimarisha kikosi cha timu yao katika safu ya ushambuliaji.

"Licha ya ugumu wa kupata mshambuliaji mzuri kwa sababu wengi wao wako katika klabu zao, lakini tumepambana na kuhakikisha tunafanikiwa kumsajili mtu ambaye atakuja kucheza na kuisaidia timu kwenye safu ya Ushambuliaji.

"Bado hatujapata mtu sahihi pale mbele wa kutufungia mabao hali ambayo Kocha wetu ametuhimiza kutafuta mshambuliaji ambaye atakuja kumaliza tatizo hilo katika kikosi cha timu yetu," alisema.

Alisisitiza kuwa msimu huu wanahitaji kuendeleza walipoishia msimu uliopita kutetea taji lao la Ligi Kuu na kuweka rekodi nzuri, Kombe la FA na kucheza nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambapo msimu uliopita walicheza fainali ya Kombe la Shirikisho.

Kuhusu baadhi ya nyota wanaohusishwa na Yanga, Sankara Karamoko, Leonal Ateba wa Cameroon na Glody Kilangalanga, alisema katika usajili hayo yapo na kuwataka mashabiki kutulia kuona wanavyosajili.

# Michezo

Jumatatu Januari 15, 2024

Nipashe




De Bruyneni gwiji City

UKURASA 21

UMESTAHILI...



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, akimkabidhi Kiungo wa Simba, Fabrice Ngoma, Tuzo ya Mchezaji Bora wa Mashindano ya Kombe la Mapinduzi baada ya mechi ya fainali dhidi ya Mlandege FC, ambayo iliibuka na ushindi wa bao 1-0 katika Uwanja wa New Amaan Complex, mjini Zanzibar juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# Benchikha ataka straika wa mabao

## Asifu michuano ya Mapinduzi kumwonesha panapovuja Simba, ageukia...

**Faustine Feliciane,** ZANZIBAR

BAADA ya kukubali kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Mlandege FC kwenye mechi ya fainali ya Kombe la Mapinduzi iliyopigwa juzi Uwanja wa New Amaan Sports Complex, mjini Zanzibar, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Abdelhak Benchikha ametema nyongo kuwa kikosi chake kinahitaji straika mwenye nguvu anayeweza kukabiliana na mabeki wawili au watatu.

**Benchikha alisema katika mchezo wa juzi wa fainali ya Komba la Mapinduzi dhidi ya Mlandege, walitengeneza nafasi nyingi lakini kukosekana kwa mshambuliaji mwenye jicho la goli kuliwafanya kushindwa kupata ushindi.**

"Tunahitaji mshambuliaji wa viwango vya juu, tulitengeneza nafasi nyingi, lakini hatukuweza kuzitumia, tunarejea kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na michezo ya Ligi Kuu, lakini kama kocha lazima niwe na mtu ambaye anaweza kutumia hizi nafasi tunazozitengeneza," alisema Banchikha.

Aidha, alisema kitu kingine alichokigundua ni udhaifu wa safu yake ya ulinzi ambayo imekuwa ikifanya makosa mara kwa mara na kuwapa faida wapinzani wao.

"Lazima tulifanyie kazi haraka, mabeki wangu wanakosa umakini sana, tunaruhusu magoli ambayo yanafanana, ni lazima tulifanyie kazi kwa sababu tuna michezo mingi mbele yetu, tunatakiwa kuwa imara," alisema Banchikha.

Kuhusu mchezo wao wa fainali dhidi ya Mlandege ambao Simba walipoteza kwa bao 1-0 na kushuhudia ubingwa ukitetewa tena na Wazanzibar hao, Benchikha alisema wapinzani wao Mlandege walitumia muda mwingi 'kupaki basi' baada ya kupata goli kwenye mchezo wao wa fainali ya Kombe la Mapinduzi juzi usiku na kuwapa ugumu.

Alisema mchezo ulikuwa mzuri lakini waliingia na mbinu ya kupaki basi ambapo wote walikuwa wakicheza nyuma ya

INAENDELEA UKURASA 23

# Yanga yatamba kupata jembe

**Na Saada Akida**

ZIKIWA zimesalia saa chache dirisha dogo la usajili kufungwa Klabu ya Yanga imetangaza kuwa inakamilisha usajili wake wa mwisho kwa kushusha mshambuliaji ambaye atakuja kuwasahaulisha mashabiki aliyekuwa straika wao kipenzi, Fiston Mayele.

Tangu ameondoka Mayele, Yanga haijapata mbadala mwingine wa nyota huyo baada ya Hafiz Konkoni aliyesajiliwa kuvaa viatu vyake kushindwa kuitendea haki nafasi hiyo, na badala yake sasa timu hiyo inategemea zaidi kupata mabao kupitia kwa viungo.

Akizungumza na Nipashe jana, Rais wa Yanga, Hersi Said, alisema wanakamilisha usajili wa mshambuliaji mpya ambaye utafunga zoezi hilo kwa kutibu tatizo la safu ya ushambuliaji kulingana na mapendekezo ya kocha Miguel Gamondi.

Alisema baada ya kufanikiwa kutambulisha nyota wawili wapya sasa mashabiki wakae mkao wa kutulia kwa sababu wako katika hatua za mwisho kushusha kifaa

INAENDELEA UKURASA 23



Miguel-Gamondi

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >